# Nipashe

**Jumanne Januari 16, 2024** Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581557

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ | nipasheTZ | The Nipashe Digital | nipasheTZ | nipashedigital | epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com




**VINICIUS JR: MIMI SI MTAKATIFU**

UKURASA 22

UKURASA WA 5

**ACT** kumwona Bashe kilio cha wakulima nchini



UKURASA WA 8

MIAKA 60 MAPINDUZI

**Majaliwa** aguswa maboresho sekta za elimu na afya



UKURASA WA 19

**Chama** tawala DRC chashinda viti vya ubunge



# Yanayomsubiri Katibu Mkuu Dk. Nchimbi CCM

• **Upinzani** wampa orodha ya mambo manne; nyumbani wataja kilichombeba... *Endelea ukurasa 2*

"Akemee makundi yanayohasimiana waziwazi ndani ya CCM. Matamshi yanayotolewa na Idara ya Itikadi na Uenezi yachujwe kabla ya kutolewa kwa jamii.
**Deus Kibamba**





"Nchimbi ana uzoefu mkubwa, anakifahamu chama na anaifahamu siasa ya Tanzania.
**Charles Kitwanga**

"Dk. Nchimbi akiingia tu ofisini aombe nyaraka za mazungumzo ya mwaka mzima kati ya CHADEMA na CCM.
**John Mnyika**





Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Rais Samia Suluhu Hassan, akimpongeza Katibu Mkuu mpya wa chama hicho, Emmanuel Nchimbi, baada ya kuteuliwa kushika wadhifa huo kwenye Kikao Maalum cha Halmashauri Kuu ya CCM Mjini Unguja, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Operesheni nyingine kuondoa ombaomba yaja Dar

UKURASA 3

## CHADEMA: CCM tuko tayari mdahalo, lakini...

UKURASA 3

**MICHEZO** **MOLOKO APISHA STRAIKA YANGA** UK.24

**KATUNI** UK.6




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza Kikao Maalum cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya chama hicho kilichokutana Mjini Unguja, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Yanayomsubiri Dk. Nchimbi CCM

**Na Waaandishi Wetu**

WAJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wameridhia pendekezo la Kamati Kuu ya chama hicho kuhusu Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kuwa Katibu Mkuu wa chama chao.

Balozi Dk. Nchimbi ambaye ameshawahi kuwa mjumbe katika kamati mbalimbali za CCM, anachukua nafasi iliyoachwa wazi na Daniel Chongolo ambaye amejiuzulu nafasi hiyo mwishoni mwa mwaka jana.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana visiwani Zanzibar, Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, alisema kufuatia kikao cha Halmashauri Kuu kilichofanyika jana visiwani humu kikiongozwa na Mwenyekiti Rais Samia, wajumbe wake wamepokea pendekezo la Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kuhusu jina la Katibu Mkuu wa CCM na wajumbe wa Halmashauri Kuu kwa sauti moja wameridhia jina hilo.

"Kwa kazi nzuri iliyofanywa, Halmashauri Kuu ya Kamati Kuu ya CCM imempongeza kwa dhati Rais wetu na Mwenyekiti wetu wa CCM, Dk. Samia kwa kazi njema anayofanya ya kutekeleza utendaji mzuri wa ilani na pia tunampongeza kwa dhati Makamu Mwenyekiti wetu na Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM," alisema Makonda.

Alisema kuwa awali kikao kilitanguliwa na semina iliyoanza Januari 3 hadi 14 mwaka huu na mambo kadhaa wajumbe walipata nafasi ya kushiriki ikiwamo mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kujua hali ya upatikanaji umeme na mpango wa serikali kuhakikisha nchi inakuwa na umeme wa kutosha.

Makonda pia alisema kuwa katika semina hiyo, wajumbe walijadili mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kujua hatua na kazi inayofanyika pamoja na Daraja la Magufuli.

Alisema wajumbe pia walijadili na kupokea taarifa ya utekelezaji wa ilani ya CCM kwa Zanzibar na kujua hali ya mashirika ya umma na mageuzi ya yanayoendelea kufanywa ndani yake.

"Pamoja na mambo mengine yote, kikao pia kilipokea taarifa mbalimbali ikiwamo maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, vijiji na vitongoji mwaka 2024, maandalizi ya maadhimisho ya Miaka 47 ya CCM ambayo yatafanyika Februari 4, mwaka huu," alisema.

**KATIBU WA 11**

Nafasi ya Katibu Mkuu wa CCM ilikuwa wazi kwa muda wa siku 48 baada ya aliyekuwa Katibu Mkuu, Chongolo, kujiuzulu nafasi hiyo na CCM kuridhia uamuzi wake huo Novemba 29, mwaka jana.

Dk. Nchimbi anakuwa Katibu Mkuu wa 11 CCM. Tangu mwaka 1977, nafasi hiyo ilishikiliwa na Pius Msekwa (1977-1982), Rashid Kawawa (1982-1990) na Horace Kolimba (1990-1995).

Wengine walioshika wadhifa huo ni Lawrence Gama kutoka mwaka 1995 hadi 1997, Philip Mangula kutoka mwaka 1997 hadi mwaka 2007, Yussuf Makamba kutoka mwaka 2007 hadi 2011 na Wilson Mukamba kutoka mwaka 2011 hadi 2012.

Abdulrahman Kinana kutoka mwaka 2012 hadi mwaka 2018, Dk. Bashiru Ally kutoka mwaka 2018 hadi mwaka 2022 na Chongolo kutoka 2022 hadi 2023.

**MZIGO WA NCHIMBI**

Waziri wa zamani wa Mambo ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Charles Kitwanga, alisema Balozi Dk. Nchimbi ni mwanasiasa mzoefu, anakifahamu chama na anajua vizuri siasa ya Tanzania.

Alisema alifurahi aliposikia Balozi Dk. Nchimbi ameteuliwa kutumikia nafasi hiyo jana.

"Binafsi nimefurahi sana kusikia Nchimbi ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM. Sina shaka naye kwa sababu ni mtu ambaye ana uzoefu mkubwa, anakifahamu chama na anaifahamu siasa ya Tanzania," alisema.

Kitwanga ambaye alikuwa Mbunge wa Misungwi katika uongozi wa Rais John Magufuli, alisema Balozi Dk. Nchimbi amefanya kazi ubalozini, hivyo ana uelewa mpana wa masuala ya kimataifa.

Mhadhiri wa Sayansi ya Siasa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Richard Mbunda, alisema Balozi Dk. Nchimbi ni mwanasiasa mzoefu na chama kipo salama chini ya uongozi wake.

"Balozi Nchimbi alishawahi kuwa Mwenyekiti wa UVCCM, ni mzoefu sana katika medani za kisiasa, nina imani naye, kwake chama kipo katika mikono sahihi kabisa, ni mtu ambaye anaweza kuleta utangamano wa kisiasa," alisema Dk. Mbunda.

Mchambuzi wa Masuala ya Kisiasa, Bubelwa Kaiza, alisema uteuzi wa Balozi Nchimbi waliutarajia kwa sababu ilifahamika kinachoendelea kwa kuwa ni mfuatiliaji wa siasa za nchini.

Alisema anafahamu ndani ya CCM kuna makundi na bado yanaendelea kuishi na anaamini Balozi Dk. Nchimbi ni mtu sahihi anayekwenda kuyamaliza.

Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, alisema Balozi Dk. Nchimbi anakwenda kukabiliana na majukumu manne katika kazi yake.

Mnyika alitaja jukumu la kwanza kwa kiongozi huyo kumshauri Rais Samia ambaye ni Mwenyekiti wa CCM, kuiondoa miswada ya sheria zinazohusu uchaguzi na masuala ya kisiasa, ukiwamo unaolenga kufanya marekebisho ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Mnyika alisema: "Jukumu la kwanza kabisa alilonalo ni kushauri Rais ambaye ni Mwenyekiti wa chama chake ili amwelekeze Waziri wa Sera, Uratibu na Bunge aiondoe hiyo miswada bungeni... amshauri ili katika Bunge lijalo upelekwe bungeni mkakati wa kuwanusuru wananchi dhidi ya ongezeko la gharama za maisha."

Kwa mujibu wa Mnyika, ili ayafanye hayo majukumu vizuri, Balozi Dk. Nchimbi, akiingia tu ofisini, jambo la kwanza anapaswa aombe kuletewa nyaraka za mazungumzo ya mwaka mzima kati ya CHADEMA na CCM.

Alisema akiyasoma, atapata mahali pa kuanzia kutokana na mapendekezo ambayo waliyawasilisha kwa nyakati tofauti kwa Rais na kwenye kamati ya mazungumzo kati ya CHADEMA na CCM.

Kamishna wa Madini wa zamani, Dk. Peter Kafumu, alisema: "He is the best (ni mtu bora) na ni chaguo sahihi kwa hali ya sasa ya nchi."

Dk. Kafumu ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Igunga Mjini katika uongozi wa Rais Magufuli, alisema Dk. Nchimbi ni mtu mzoefu katika siasa, alianzia UVCCM, amekuwa serikalini na amekuwa balozi.

Mtaalamu huyo wa Jiolojia alisema kwamba chama kilikuwa kinamhitaji mtu kama Balozi Dk. Nchimbi wakati wa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025

Askofu Prof. Victor Chisanga, alisema Dk. Nchimbi anaweza kuacha alama kama atakishawishi chama chake kiridhie kuandika Katiba Mpya, nchi iwe na Tume huru ya Uchaguzi na kuziba mianya ya ufujaji wa fedha za umma.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maadili, Amani na Haki za Binadamu kwa Jamii ya Viongozi wa Dini, Askofu William Mwamalanga, alisema kazi kubwa aliyonayo Dk. Nchimbi ni kurejesha imani ya CCM kwa wananchi.

Mhadhiri kutoka Chuo cha Diplomasia, Deus Kibamba, alisema ana imani na Balozi Dk. Nchimbi kwa sababu ni jina ambalo limejitokeza mara nyinyi na anamwona anafaa kutokana na historia yake ndani ya chama.

Alisema Dk. Nchimbi atakuwa na jukumu la kurudisha ustahimilivu na uwajibikaji ndani ya chama hicho.

Pia alisema jukumu lingine litakalomtazama Dk. Nchimbi ni kurudisha taasisi ndani ya CCM, kukemea makundi yanayohasimiana waziwazi ndani ya chama na kuhakikisha matamshi yanayotolewa na Idara ya Itikadi na Uenezi yanachujwa kabla ya kutolewa kwa jamii.

***Imeandaliwa na Rahma Suleiman (ZANZIBAR), Beatrice Shayo, Elizabeth Zaya, Maulid Mbaga, Restuta James (DAR)**

HABARI KITAIFA

# Operesheni nyingine kuondoa ombaomba yaja Dar es Salaam

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ameagiza kukamatwa na kuondolewa ombaomba wote kwenye mitaa mbalimbali mkoani mwake, wakiwamo wenye ulemavu.

Aliagiza hayo jana wakati wa mkutano wake na watendaji wa serikali kuhusu tahadhari dhidi ya magonjwa ya mlipuko na kuwapo taarifa za maandamano yanayotarajiwa kufanywa na wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Januari 24, mwaka huu.

Ni hatua ya aina hiyo inayorejea kwa mara nyingine huku hatua kama hizo zikiwahi kuchukuliwa na baadhi ya waliokuwa wakuu wa mkoa huo, akiwamo John Mhavile katika miaka 1980 kupitia 'Operesheni Nguvu Kazi'.

Viongozi wengine katika miaka ya karibuni walioondoa ombaomba kwa nguvu ni Yusuf Makamba, Paul Makonda na Abubakar Kunenge. Vilevile, aliyekuwa Naibu Waziri - TAMASEMI, Joseph Kakunda alishalitekeleza hilo.

Katika tamko la jana, Chalamila aliagiza kazi ya kuondoa ombaomba ifanyike haraka na kwa kuwa imebainika kuna baadhi ya watu wanaowatumia watu wenye ulemavu kujipatia kipato.

"Kuna watu wanazagaa kwenye Daraja la Tanzanite, kamateni watu wote ambao mtawakuta wakiwa na watu wenye ulemavu kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam wakiomba.

"Tumegundua ule ni mtaji wa watu ambao jioni wanakusanya mapato halafu wanawapatia kidogo wale wenye ulemavu.

"Kwahiyo, wenye ulemavu wote wanaomba waondolewe barabarani. Rais Samia Suhulu Hassan (serikali) ametoa fedha kwa ajili ya nyumba za watu wenye ulemavu na watakaoendelea kuomba wakamatwe."



Kuhusu maandamano yaliyoitishwa na CHADEMA, Chalamila alisema hana taarifa kuhusu tukilo hilo na kwamba anachofahamu siku hiyo ni maalum kwa ajili ya kufanya usafi.

Alisema anayepaswa kutoa taarifa za kuwapo maandamano ni Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro.

Hata hivyo, mara kadhaa serikali imetoa agizo la kuondolewa makundi ya watu wanaoomba msaada katika makutano ya barabara na mitaa ya Jiji la Dar es Salaam.

Mwaka 2021, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo, Kunenge alitoa agizo kama hilo, akionya kuwa ongezeko la ombaomba kwenye mkoa huo linatokana na baadhi ya watu wasio waaminifu ambao huwasafirisha watu wenye ulemavu kutoka mikoa mbalimbali na kuwaleta jijini kwa ajili ya kazi hiyo kwa manufaa yao.

Mbali na Chalamila na Kunenge, viongozi wengine waliowahi kutoa agizo hilo ni aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Joseph Kakunda, ambaye alisema ombaomba wengi wamekuwa wanakwenda katika mkoa huo kutokana na vivutio vingi vinavyowapa nafasi ya kupata fedha kama sehemu ya ibada.

Alisema kuwa mara nyingi ofisi ya mkoa huo zimekuwa zinachukua hatua ya kuwaondoa kwa kuwarejesha makwao, huku akitolea mfano kwamba mwaka 2013 ombaomba 253 na watoto 135 walirejeshwa kwao, huku watoto 32 wakirejeshwa shuleni.

Kakunda pia alisema kwamba wapo watu wazima ambao wamekuwa wanawatumia watoto na watu wenye ulemavu kuomba kwa ajili ya kujinufaisha wenyewe.

# Chadema yakubali mdahalo na CCM

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema kipo tayari kushiriki mdahalo na Chama Cha Mapinduzi (CCM), huku kikitoa masharti matano.

Kimetaja masharti hayo kuwa ni kuondolewa miswada mitatu iliyowasilishwa bungeni inayohusu sheria za uchaguzi, kuanzishwa mchakato wa marekebisho ya Katiba ya Mwaka 1977, serikali iwasilishe bungeni Muswada wa Sheria ya kukwamua mchakato wa Katiba mpya na jibu la lini nchi itapata Katiba mpya.

Kimetoa masharti hayo baada ya juzi Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda alipokuwa Unguja, kutaka kufanyike mdahalo wa wazi kati yake na viongozi wa CHADEMA ili Watanzania wachague ikiwa wataendelea na maandamano au kuchagua maridhiano.

Kauli hiyo ya Makonda ilikuja siku moja baada ya Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Freeman Mbowe kutangaza maandamano ya amani Januari 24.

Jana chama hicho kupitia kwa Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje, John Mrema, kilisema wapo tayari kushiriki.

Mrema alisema msimamo wa chama hicho katika kushiriki mdahalo huo ni endapo CCM itatekeleza masuala waliyoweka msimamo.

"Ili mdahalo huo ufanyike tunataka ulenge kuhusu kuishauri serikali jinsi ya kupunguza ukali wa gharama za maisha na kuonyesha kodi na tozo zipi zipunguzwe, anasa gani ziondolewe na serikali, na mkakati mzima wa kupunguza ukali wa gharama za maisha kwa wananchi.

"Tunamkumbusha Mwenezi wa CCM kuwa miswada hii imepelekwa bungeni na serikali na imepuuza maoni ya wananchi, viongozi wa dini, wadau wa vyama vya siasa, ripoti za waangalizi wa uchaguzi wa kimataifa na ndani, taarifa ya NEC ya mwaka 2020 pamoja na amri za Mahakama ya Afrika na Afrika Mashariki kuhusu maeneo mahsusi ya kuboresha mifumo ya uchaguzi na sheria ya vyama," alisema Mrema.

Alisema katika kipindi hiki (Makonda) aweke mdahalo ili serikali ione ulazima wa kusikiliza na kuheshimu maoni ya wananchi na wadau mbalimbali wa chaguzi katika kuandaa mazingira bora ya kuwa na chaguzi huru na haki nchini.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

TAWA

**INVITATION FOR BIDS (IFB)**

**TANZANIA WILDLIFE AUTHORITY (TAWA)**

**Project: Selous Ecosystem Conservation and Development Programme (SECAD)**
**(KfW Contract Reference No.:2012 66 451)**
**16TH January 2024**

1. The **Government of the United Republic of Tanzania** has received a grant from the **German State–Owned Investment and Development Bank (KfW) towards the costs of implementing the Selous Ecosystem Conservation and Development Programme (SECAD),** and intends to apply part of the proceeds towards payments under the contract for **Construction of Rural Infrastructure (i.e., Socio-economic Infrastructures) in Selous Game Reserve (SGR).**

2. The **Tanzania Wildlife Authority (TAWA)** now invites sealed bids from eligible and qualified bidders for the construction works comprised of various rural Socio-economic Infrastructures as shown in the table below:

| Package Number | Tender Number | Procurement Plan Number | Tender Description |
|---|---|---|---|
| **014** | MNRT/GOPA/KINGUPIRALOT1PP09 | PP 09 | Construction of Drainage Structures for Selous Game Reserve at Kingupira Sector |

***Note:***

3. Bidding will be conducted by means of the National Competitive Bidding (NCB) procedure with the qualification as specified in the KfW Guidelines for Procurement of Goods, Works and associated Services in Financial Cooperation with Partner Countries ("KfW Guidelines" **https://www.kfw-entwicklungsbank.de/PDF/Download-Center/PDF-Dokumente-Richtlinien/FZ-Vergaberichtlinien-V-2021-EN.pdf).**

4. A complete set of the bidding documents **(in English)** is available to interested eligible Bidders upon the submission of a written application to the address below and upon payment of a non-refundable fee of ***Tanzanian Shillings One Hundred Thousand only (TZS100,000.00)*** or its equivalent in freely convertible currency for each set (per tender reference number). The method of payment is via bank deposit to the following account at **Tanzania CRDB bank – Account name: Selous Ecosystem Conservation and Development with Account number 0150555174201.**

The documents shall be sent by Courier (related costs to be covered by the interested Bidder) or physical pickup by the Bidders at ***Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT), c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No. L406, PO Box 25295, 40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania.***

5. Bids in one original plus two paper copies and one digital copy, properly filled in, and enclosed in plain envelopes must be delivered to the address below: ***SECAD Project Manager, Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT), c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No. L406, PO Box 25295, 40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania*** on or before **Wednesday 7th *February 2024 at 12:00 hours* EAT**. Electronic bidding will not be permitted and late bids will be rejected. Bids will be publicly opened in the presence of the bidders' or designated representatives and anyone who choose to attend at the address below on **Wednesday 7th *February 2024 at 14:30 hours*** at ***MNRT Room No. L406.***

**Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT)**
**c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No.L406, PO Box 25295,**
**40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania.**
**Contact: - SECAD Project Coordinator**
**Email:- SECADtenders@gopa-infra.de**

# Wawili wanaosadikiwa majambazi wauawa wakishambuliana na polisi

Na Gideon Mwakanosya, SONGEA

WATU wawili wanaosadikiwa kuwa majambazi wamefariki dunia wakati wakishambuliana na polisi waliokuwa doria wilayani Tunduru, Mkoa wa Ruvuma wakati wakijiandaa kwenda kufanya uhalifu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Alfred Husein alisema, tukio hilo lilitokea Januari 14, mwaka huu majira ya saa 3:30 usiku Kijiji cha Msagula nje kidogo ya makao makuu ya Tunduru.

Alisema, inadaiwa siku ya tukio polisi mkoani humo kupitia idara ya upelelezi kesi za jinai kitengo cha kuzuia na kutanzua uhalifu, walipata taarifa toka kwa wasiri wao kuwa katika kijiji cha Msagula kuwa kuna watu wawili wenye silaha wanaosadikiwa kuwa majambazi, wakiwa na pikipiki ambayo haina namba za usajili wakitokea Tunduru kwenda kijiji hicho kujiandaa kwenda kufanya uhalifu wa unyang'anyi wa kutumia silaha katika maduka ya huduma za fedha.

Alisema baada ya polisi kupata taarifa hiyo walianza ufuatiliaji wa haraka na kuandaa mtego kwa ajili ya kufanikisha kuwakamata na baada ya watu hao kufika kwenye eneo lililokusudiwa kufanya uhalifu waligundua kuwa wanafuatiliwa na polisi ndipo walipoanza kufyatua risasi hewani na polisi walijibizana nao na kufanikiwa kuwajeruhi kwa kuwapiga risasi maeneo mbalimbali ya miili yao na kuwakamata wote wakiwa na silaha moja ya kivita aina ya AK 47 ambayo imefutwa namba za usajili ambayo ilikuwa na risasi 14 ndani ya magazine pamoja na simu mbili aina ya ITEL viswaswadu.

Alisema jitihada za kuwakimbiza majeruhi hao kwenda hospitali zilifanyika na kwa bahati mbaya walifariki dunia wakati wakipatiwa matibabu na kwamba miili yao imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhiwa maiti kwa ajili ya utambuzi.

Kamanda Husein alisema kuwa jeshi linatoa wito kwa wananchi kutojihusisha na vitendo vya uhalifu na kutoa rai kwa wananchi wote wa Mkoa wa Ruvuma kuendelea kutoa taarifa za wahalifu ili waweze kushugulikiwa kwa mujibu wa sheria.



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma (kulia), akisalimiana na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Nassor Shaaban, wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika viwanja vya Nyamanzi mjini Unguja, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCAA yazuia ndege za Kenya kutua Tanzania

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imetangaza kuzuia kutua nchini ndege za Shirika la Ndege la Kenya (KQ) kuanzia Januari 22, mwaka huu.

Hadi sasa KQ inafanya safari zake kutoka jijini Nairobi kuja Dar es Salaam mara 33 kwa wiki.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Hamza Johari ilibainisha kuwa hatua ya kuzuia ndege za KQ kutua nchini ni kutokana na Kenya kuzuia ndege ya mizigo ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kutua nchini humo.

Alisema hatua ya Mamlaka ya Ndege Kenya kuzuia ndege ya mizigo ya Tanzania kutua nchini mwao imevunja Ibara ya 4 ya mkataba wa makubaliano ambayo nchi hizo zilingia mwaka 2016.

"Hatua hii ni kulipiza baada ya Mamlaka ya Kenya kukataa ndege ya mizigo ya ATCL kutua kwao licha ya vielelezo vyote vya mkataba huo," alisema Hamza katika taarifa yake kwa umma.

Zaidi alieleza kuwa Tanzania inaheshimu na kusimamia makubaliano ya kimataifa ya masuala ya anga ambayo imeingia.

"Serikali ya Tanzania siku zote inaheshimu makubaliano ya Chicago ya mwaka 1994 kuhusu makubaliano ya usafiri ya anga baina ya nchi mbili," alisema Johari.

Hatua ya kuzuiliwa kwa ndege za KQ kutua hapa nchini kutaleta athari kwa mamia ya wasafiri kwa sababu wengi hutegemea mashirika hayo katika safari.

Maelfu ya abiria wanategemea safari za kibiashara, utalii na familia, hivyo kuzuiliwa kwa safari kwa mashirika hayo kutaleta athari kubwa.

Mgogoro kati ya Tanzania na Kenya katika masuala ya anga si mpya. Agosti mwaka 2022, Tanzania ilizuia ndege za KQ baada ya Kenya kuiondoa Tanzania kutoka orodha ya nchi ambazo raia wake wanaingia nchini humo pasipo kuwekwa karantini.

Hata hivyo, zuia hilo liliondolewa lakini mvutano baina ya nchi hizo ulikuwa bado mkubwa.

# TAWA yaiagiza Manyoni kuendesha karakana kisasa

Na Christina Haule, MANYONI

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), imeuagiza uongozi wa karakana ya kanda ya kati Wilaya ya Manyoni, mkoani Singida iliyojengwa kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 217 kuweka mfumo madhubuti na usimamizi ikiwamo wataalamu wa vifaa vya kisasa ili iendeshwe kisasa zaidi.

Kamishna wa Uhifadhi wa TAWA Mabula Misungwi Nyanda, alisema mwishoni mwa wiki wakati akiwa kwenye ziara Kanda ya Kati wilayani Manyoni kukagua shughuli za uhifadhi na utalii zinazotekelezwa wilayani humo.

Nyanda alisema ubora wa viwango vya ujenzi wa karakana ya matengenezo ya magari na mitambo iliyojengwa katika kanda hiyo ni kubwa kuliko zote zilizojengwa na taasisi hiyo nchini.

"Nimetembelea na kukagua karakana, kimsingi nimeona imejengwa vizuri na pia nimeona ina uwekezaji mkubwa wa vifaa vitakavyotumika na nina imani hii karakana itatusaidia sana," alisema.

Kamishna Mabula alisema Manyoni ni katikati ya nchi na ni sehemu inayofikika kwa urahisi, na kutokana na ukubwa wake itatumika kutengeneza magari ya taasisi nzima.

Aidha, alihimiza maofisa na askari wote wa TAWA kurejea mpango mkakati wa taasisi hiyo ambao unafikia kikomo mwaka 2026 utakaowasaidia kutekeleza na kufikia majukumu yao ipasavyo.

Alifafanua kuwa mpango mkakati wa TAWA una malengo makuu matatu ambayo ni kuhakikisha rasilimali ambayo TAWA imepewa kusimamia inakuwa salama, pia kuhakikisha wateja wote wa taasisi wakiwamo wawekezaji wanapata huduma na kuridhika na huduma inayotolewa na lengo la tatu ni kufanya kazi kwa ufanisi na tija.

Alisisitiza kuwa malengo hayo hayataweza kutimia bila kuishi katika tunu za taasisi hiyo ambazo ni uadilifu, kufanya kazi kwa ushirikiano, kutenda kazi kwa ubunifu pamoja na kufanya kazi kwa juhudi na maarifa.

Naye Kamishna Msaidizi Ulinzi wa Rasilimali za Wanyamapori, Hadija Malongo aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia TAWA kwa kuwezesha ujenzi wa karakana hiyo ambayo kukamilika kwake kutasaidia kupunguza gharama za matengenezo ya magari ambayo ilikuwa changamoto kubwa.

# Dar yaongoza idadi wagonjwa wa macho

Na Maulid Mmbaga

WIZARA ya Afya imesisitiza wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa macho 'Red eyes' ulioibuka nchini hivi karibuni na ambao unatajwa kuathiri baadhi ya watu huku Dar es Salaam ikitajwa kuongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa ambao ni 869.

Wito huo ulitolewa jana kupitia taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Huduma za Tiba kutoka Wizara ya Afya Prof. Pascal Ruggajo kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu iliyolenga kutoa taarifa ya uchunguzi wa awali ya ugonjwa huo.

Prof. Ruggajo alisema dalili ya ugonjwa huo ni pamoja na macho kuwasha, kuchoma choma, kuuma, kutoa machozi na tongo tongo za njano, hali ambayo inaripotiwa kuonekana kwa baadhi ya watu nchini.

"Taarifa za uchunguzi zinaonyesha maambukizi ya kirusi hiki kwenye ngozi ya juu ya gololi ya jicho ni maambukizi yanayosambaa kwa kasi kubwa. Hakuna tiba maalumu kwa ugonjwa huu na hata bila tiba dalili huisha zenyewe ndani ya wiki mbili," alisema Prof. Ruggajo.

Aliongeza kuwa mwenendo wa ugonjwa huo unaonyesha kuna ongezeko kubwa la wagonjwa wanaofika katika vituo vya kutolea huduma za afya wakiwa wanasumbuliwa na ugonjwa huo.

"Katika kipindi cha Desemba 22, 2023 hadi Januari 11, mwaka huu kumekuwa na ongezeko kubwa la watu wanaosumbuliwa na ugonjwa huu kufika katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya matibabu, kwa mfano katika mkoa wa Dar es Salaam kuna wagonjwa wapya 869 huku hali ya kawaida katika kipindi cha mwezi Desemba 2023 kulikuwa na wagonjwa 17 pekee," alisema Prof. Ruggajo.

Aidha, alisisitiza kuwa suala la usafi ni jambo muhimu katika kuzuia maambukizi kusambaa kwa wengine kutokana na tabia ya ugonjwa huu kusambaa kwa kasi, na kwamba maambukizi hayo huleta mlipuko ambao husambaa kupitia kirusi kwa asilimia zaidi ya 80.

Hata hivyo aliwashauri wananchi kutokutumia dawa zisizo rasmi na ambazo hazijaandikwa na daktari kwa wakati huo na kutotumia dawa za macho anazotumia mgonjwa mwingine ili kuepuka madhara kwa kuwa dawa za macho ni tofauti na zinatolewa kwa matumizi tofauti.

HABARI KITAIFA




Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, akipata maelezo kutoka kwa Meneja Uhusiano wa Benki ya Azania, Majaba Magana, alipotembelea banda la benki hiyo kwenye maonyesho ya Kimataifa ya Biashara Zanzibar. Benki ya Azania ni mmoja wa wadhamini wa maonesho hayo yanayoendelea katika kituo cha kimataifa cha Dimani-Fumba jijini Zanzibar. Katikati ni Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# LATRA yataka watoa huduma katika mabasi wapatiwe mafunzo

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) imewataka wenye mabasi kupeleka watoa huduma wa magari yao kupata mafunzo ya huduma kwa wateja ili watoe huduma bora na hivyo ikukuza biashara zao.

Ni rai iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Udhibiti wa Usafiri wa Barabara LATRA, Johansen Kahatano wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa watoahuduma wa mabasi huko Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

"Wasafirishaji tunawaomba wawezesheni wafanyakazi wenu wasome mafunzo haya, hatuwalazimishi muwalipie, lakini walipieni hata kwa mkopo wasome kwa sababu wakisoma wanaongeza thamani kwenye baishara yako, na huduma zikiwa bora mtapata wateja wengi," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema usalama wa abiria ni muhimu, hivyo kama watoahuduma watapata mafunzo, watahakikisha abiria wote wanafunga mikanda wakati wote wa safari.

"Watoahuduma wengi wa mabasi hawafungi mikanda, wanawaambia abiria wafunge mikanda lakini wao hawafungi mikanda, lazima mtambue kuwa na ninyi mnatakiwa kukaa kwenye viti na kufunga mikanda ili muwe mfano kwa mnaowaambia wafunge mikanda kwa usalama wao," alisema.

Kahatano alisema watoahuduma wafundishwe namna ya kushughulikia malalamiko ya wateja ili wajue mteja anapokuwa na malalamiko kwake anataki wa kufanya nini.

"Sheria inatutaka sisi LATRA tulinde mitaji ya wateja wetu. Kwahiyo, mafunzo kama haya ni sehemu ya kulinda mitaji ya wateja wetu kwa sababu huduma zikiwa bora, biashara zao zitaendelea kukua," alisema.

Mkuu wa CBE, Prof. Edda Lwoga, alisema katika kuunga mkono juhudi za serikali, CBE imeamua kutoa mchango wake katika kukuza weledi na ufanisi wa watoahuduma wa usafiri wa umma.

Alisema lengo ni kuhakikisha huduma hizo zinakuwa na ubora wa hali ya juu na kwamba CBE ni miongoni mwa taasisi ambazo zimepewa kibali cha kutoa mafunzo hayo.

Alisema tayari chuo kimeshaandaa mitaala, mwongozo wa mafunzo, wawezeshaji na vitendea kazi vyote muhimu kwa mafunzo hayo.

"Ni matarajiio yetu kuwa mara tu baada ya uzinduzi huu chuo kitaanza rasmi udahili wa washiriki wa mafunzo na yatafanyika katika vituo vilivyoko katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya," alisema.

Aliongeza kuwa CBE inatambua juhudi zilizofanywa na serikali kupitia LATRA katika kuboresha usafiri wa barabara nchini.

Alisema kuanzishwa kwa LATRA kupitia Sheria ya Udhibiti wa Usafiri ya Mwaka 2019, ni hatua muhimu katika kusimamia na kuboresha sekta hiyo muhimu.

"Hata hivyo, bado tunashuhudia sekta hii ikiendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile uvunjifu wa sheria na kanuni za usalama barabarani, huduma kwa wateja zisizoridhisha, hali hii inahitaji jitihada zaidi kutoka kwa wadau wote," alisema.

Mkuu wa Dawati la Elimu ya Usalama Barabarani wa Jeshi la Polisi, Michaek Deleli, alisema jeshi hilo linaona mafunzo hayo ni fursa kubwa kwa sababu yataondoa changamoto nyingi za barabarani kwenye usafiri wa umma.

"Kuna mambo yanafanyika ya kiuhalifu kwenye usafiri wa umma na yanatokana na watoahuduma kutokuwa na elimu sahihi, mfano tumeshuhudia kusafirishwa kwa wahamiaji haramu, vitendo vinafanywa na watoahudumu wasio na mafunzo wala kujua sheria za nchi," alisema.

Aliongeza kuwa hata dawa za kulevya zinasafirishwa kupitia magari, hasa mabasi lakini yanapokamatwa watoahuduma wanashindwa kuwatambua wamiliki, hali ambayo imekuwa inasababisha changamoto.

Mweka Hazina wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Mbazi Mjema, alipongeza serikali kwa uamuzi wa kuanzisha mafunzo hayo kwa kuwa yatasaidia chama hicho kutimiza majukumu yake na utendaji wa kazi utaboreshwa.

"Tuna wafanyakazi wengi wa darasa la saba, hivyo vyeti watakavyopata ni mali yao. Wakihama kampuni moja kwenda nyingine cheti kinabaki kuwa mali yao binafsi. Tupunguzieni ada ya mafunzo ili tuweze kuwapeleka mafunzo watoahuduma wengi," alisema.

# ACT yabeba hoja za wakulima, kuziwasilisha kwa Waziri Bashe

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kimeorodhesha changamoto zinazowakabili wakulima na kitaziwasilisha kwa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe ili zitatuliwe.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Zanzibar, Othman Masoud Othman, alibainisha hayo jana wakati wa mkutano uliokutanisha wajumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho mkoani Ruvuma.

Alisema miongoni mwa changamoto ambazo wamepanga kuziwasilisha kwa Bashe ni kuhusu upatikanaji na usambazaji pembejeo na ununuzi wa mazao.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar alitolea mfano Ruvuma, akisema haoni haja mkoa huo kuendelea kuwa maskini ilhali umebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi ikiwamo ardhi yenye rutuba na vyanzo vya maji.

"Nimepokea changamoto katika ziara hii, lakini nyingi ni kuhusu wakulima hususani katika eneo la upatikanaji, usambazaji wa pembejeo na ununuzi wa mazao. Nitazifikisha kwa viongozi wenye dhamana serikalini akiwamo Waziri Bashe.

"Licha ya jitihada ambazo serikali imezichukua kwenye upatikanaji na usambazaji pembejeo hizo, bado hali si shwari kwa wakulima wa Ruvuma hasa kwenye eneo la upatikanaji mbolea.

"Katika msimu uliopita wa kilimo, badala ya kugawa vijijini waliko wakulima, inagawiwa mjini na imekuwa haipatikani kwa wakati," alisema.

Othman alisema licha ya ahadi ya serikali kununua mahindi tani 500,000 kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), wakulima hawakuuza mazao yao kwa bei nzuri na hawakulipwa kwa wakati.

"Sisi ACT-Wazalendo, hoja yetu ni kwamba serikali inapaswa kuimarisha bajeti na uwezo wa NFRA na Kampuni ya Taifa ya Mbolea (TFC) ili kuwanusuru wakulima wa Ruvuma na Tanzania kwa ujumla," alisema Othman.

Kiongozi huyo anaendelea na ziara yake ya ujenzi wa chama katika mikoa ya Ruvuma, Lindi, Mtwara, Dar es Salaam pamoja na mkoa wa kichama Selous unaojumuisha majimbo ya Tunduru Kusini, Tunduru Kaskazini na Namtumbo.

Mbali na Othman, viongozi wengine wa ACT-Wazalendo wametawanyika katika mikoa mbalimbali wakifanya mikutano yao ya kujenga chama hicho akiwamo mjumbe wa Kamati Kuu, Ismail Jussa, aliyeko Mkoa wa Singida.

Wengine ni Mwenyekiti, Juma Duni Haji, aliyeko Mkoa wa Mara pamoja na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Tanzania Bara, Dorothy Temu.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
15.01.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **21.01.2024 hadi 27.01.2024** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha magari matupu wenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga kuelekea Bandari ya Dar Es Salaam,** gari hilo lenye namba za usajili. **NRB97300 / NRB15200 DS00TG-GP/ NRB43293**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita** | **36.5** |
| **Upana** | - | **Mita** | **4.30** |
| **Kimo** | - | **Mita** | **4.60** |

3. Njia itakayotumika: **Mzenga hadi Bandari ya Dar Es Salaam** kupitia Barabara ya Morogoro, Barabara ya Mandela gari litasafiri muda wa mchana ***( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117786202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuwasha mtambo Bwawa Mwalimu Julius Nyerere leo ni habari njema

**LEO** Shirika la Umeme (TANESCO) linatarajia kuwasha mtambo mmoja wa kuzalisha umeme wa Megawati 235 kutoka kwenye Bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere (JNHPP) na kuingizwa kwenye gridi ya taifa.

Habari hizi zinaleta matumaini ya upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini ambao utachochea uwekezaji katika maeneo mbalimbali na kukuza uchumi wa nchi.

Bwawa hilo ni matumaini makubwa kwa Watanzania na wawekezaji wanaokuja nchini kufanya uwekezaji wa uhakika na kuondokana na adha ya kukatika mara kwa mara kwa nishati hiyo.

Wakati mradi huo ulipoanza kujengwa Watanzania walielezwa kuwa utaondoa kabisa tatizo la umeme na itabaki kuwa historia.

Kwa mujibu wa Tanesco, wameshaanza awamu ya pili ya maandalizi ya kupokea umeme kutoka katika bwawa hilo kwa kuunganisha kituo kipya cha kupoza umeme wa 400kV Chalinze na njia ya Msongo wa Kilovoti 220 inayoanzia Luguruni hadi mkoani Morogoro.

Shirika hilo lilifahamisha kuwa maandalizi ya kupokea umeme wote utakaoanza kuzalishwa na JNHPP kuanzia tarehe 16 mpaka tarehe 19 yamefanyika na wanajizatiti kwa mifumo na hii ni awamu ya pili ya megawati 235 za mashine zinazoenda kufanyiwa majaribio zitakazokuwa na uwezo wa kuingizwa kwenye gridi ya taifa.

Kwenye taarifa yake kwa vyombo vya habari mwishoni mwa wiki, Shirika hilo lilisema limeanza awamu ya pili ya maandalizi ya kupokea umeme kutoka kwenye mitambo ya kufua umeme ya bwawa hilo na kuuingiza kwenye gridi ya taifa.

Ilisema kazi hiyo itakapokamilika itaongeza uwezo wa Kituo cha 400kV Chalinze kupokea umeme utakaozalishwa kwenye mitambo ya bwawa hilo na kuingizwa kwenye gridi ya taifa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, zoezi hilo lilianza Jumamosi tarehe 13 na linatarajiwa kukamilika Januari 21 na kwa kipindi kazi hiyo inapoendelea kutakuwa na athari za kutopatikana kwa umeme kwa nyakati tofauti.

Maeneo yatakayoathirika ni yaliyounganishwa na gridi ya taifa kwasababu njia ya msongo wa kilovolti 220 kutoka Luguruni kwenda Morogoro itazimwa na kuingia kwenye kituo cha kilovolti 400 Chalinze.

Katika kipindi hiki ambacho Shirika linafanya maunganisho ni vema wananchi wakawa wavumilivu kwasababu imeelezwa athari itakayojitokeza ya kutopatikana umeme wa kutosha katika baadhi ya maeneo.

Bwawa la JNHPP lina mitambo tisa ambayo kila mmoja utakuwa na uwezo wa kuzalisha Megawati 235 na kwa ujumla itakapoanza itazalisha Megawati 2,115 za umeme hivyo kuondoa kabisa tatizo la umeme kwenye maeneo yote nchini.


Ujenzi wa bwawa hilo ambalo liko kwenye hatua za mwisho kwa sasa umevuka asilimia 92 na ulianza kutekelezwa mwaka 2018.

Alipotembelea mradi huo hivi karibuni, Naibu Waziri Mkuu, Doto Biteko alisema serikali inafurahi kuona kwamba mkandarasi ameshalipwa asilimia 85 ya fedha za kutekeleza mradi huo na kwamba anaamini utakamilika hivi karibuni na kuondoa shida ya umeme.

Watanzania wanatarajia ile ndoto waliyokuwa wakiisubiri kwa muda mrefu wa kuondokana na tatizo la kukatika umeme mara kwa mara sasa inaondoka.

Pia, matarajio yao makubwa ni kuona treni ya kisasa (SGR) itakapoanza safari zake haitapata changamoto ya umeme.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ndiyo mafunzo ya amali ni muhimu

Na Mwandishi Wetu

**TEKNOLOJIA** ni jambo lisilokwepeka ni kama wakati huwezi kuukimbia, hivyo ni zama za kuishi na kutumia teknolojia, jambo linaloisukuma serikali kupopanua wigo kwenye taaluma za ufundi au amali.

Ni miaka ambayo elimu ya amali na ufundi inapewa msukumo mpya. Ni jambo jema kwa kuwa Tanzania inafanya mambo mengi yanayohitaji wataalamu na mafundi kufanyakazi nyingi zinazoibuka sasa.

Kwa mfano, kutafiti na kuchimba gesi na mafuta hivyo mitaala na ujifunzaji una jukumu la kujielekeza kufunza na kuanzisha utaalamu utakaofanikisha kupata mitambo ya kutoboa miamba kufikia maji, mafuta na gesi kwenye miradi hiyo.

Ni vyema kuzingatia kuwa wasomi wanaoandaliwa kwenye sekondari na vyuo waje na utaalamu wa kupasua miamba na kuivunja ili kufikia gesi na mafuta ambavyo ni muhimu kwenye maendeleo ya uchumi wa taifa.

Si hivyo tu, taifa pia limeingia kwenye teknolojia ya usafirishaji wa kileo zaidi, mfano ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR, ni wazi vitahitajika vipuri kwa ajili ya mabehewa, reli na shughuli za uchukuzi hivyo amali ijielekeze kujibu hitaji hilo kwa kuzalisha wataalamu wa hapa nchini watakaochonga na kutengeneza bidhaa hizo.

Wakati huu ni wa kukabili mabadiliko ya tabianchi, magari yanabadilishwa kuelekea injia za gesi na kuondoka kwenye mafuta, mafunzo ya vyuo vya ufundi kadhalika yajikite kwenye kuchonga vipuri vya magari na mitambo, ambayo vitatumia gesi na si mafuta yanayoelekea kuondolewa.

Kuandaa wataalamu watakaotoa huduma za kiuhandisi katika nyanja tofauti kwenye kampuni na karakana za umma na binafsi ni jambo la kupewa kipaumbele wakati huu wa kufundisha mtaala wenye mafunzo ya ufundi.

Ni habari njema kuwa mafunzo yanaanza wakati taifa hasa Zanzibar ikiwekeza kwenye uchumi wa bluu unaohusisha bahari jambo linaloanzisha mkakati wa kutoa elimu itakayofanikisha utekelezaji wa miradi ya viwanda vya samaki na kufikia rasilimali za baharini kwa wepesi.

Ikumbukwe Tanzania inapokea, kutumia na kutupa tani nyingi za simu za mkononi zenye viambato(accessories) kuanzia chuma, plastiki, madini mbalimbali na vioo.

Ni wakati wa kutafuta na kuibua mbinu mpya za kiufundi za kuyeyusha viambato na kupata bidhaa mbalimbali bora kutoka kwenye mabaki au taka za simu.

Kilimo na umwagiliaji ni kazi inayohitaji matumizi ya teknolojia na ubunifu, miji na majiji yana majitaka yanayohitaji kusafishwa, kutolewa sehemu moja na kupelekwa eneo jingine na kuyaongezea thamani iwe kuyatumia viwandani au mashambani.

Ni kazi ya shule na vyuo kuandaa wataalamu hao watakaoshughulikia majitaka hayo na kuongeza thamani kwenye kazi za uzalishaji.

Kutokana na kukua kwa teknolojia watu wengi wamekuwa wakiagiza mashine mbalimbali kutoka nje ya nchi hali ambayo inahitaji kurekebishwa, biashara hiyo ibaki Tanzania kwa kuandaa wataalamu kwenye amali ambao watatengeneza mitambo hiyo na mashine ambazo zinaagizwa nje.

Huo utakuwa ukombozi kiuchumi kwasababu nchi itaachana na kuagiza bidhaa au mashine mitumba kutoka ng'ambo.

Matumizi ya teknolojia yafanikishe kupata njia bora za kuchakata taka mitaani, kuziondoa kwa wepesi barabarani, kuimarisha usafi kwenye mitaro ya maji barabarani, vyuoni, hospitalini, shuleni na viwandani ili kuleta wepesi na ufanisi.

Ikumbukwe Tanzania na Zanzibar kuna mahitaji makubwa ya kuchomelea, kukarabati, kuyeyusha chuma, kuunga, kukisafishaji na kukipa matumizi mengine bora kwenye gereji, viwandani na karakana mbalimbali ni eneo ambalo serikali inapoanza kufundisha amali shuleni na vyuoni liboreshwe na kuongeza tija zaidi.

Tanzania inapojikita kwenye kuendeleza sayansi na teknolojia na kuongeza ujuzi wa mafunzo amali iwe na mipango ya kuchimba na kuyeyusha chuma kilichoko Liganga mkoani Njombe.

Kwa kuwa na sifa ya kuwa na rasilimali hiyo kuwe na tanuru la kuyeyusha chuma ambalo wateja kutoka Afrika Masharika kama Uganda, Kenya na DRC watakuja kutumia huduma hiyo.

Mafunzo ya amali vyuoni na shuleni yawe na tija kwa kuziba mapengo na kupunguza upungufu uliokuwapo kwenye maeneo mbalimbali.

# Mwanafunzi adaiwa kujiua kwa kupoteza 61,000/-

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MWANAFUNZI wa kidato cha tatu Shule ya Sekondari Mazinge, Manispaa ya Shinyanga, Joyce Hezron (17), adaiwa kunywa sumu na kusababisha kifo chake baada ya kupoteza Sh. 61,000 aliyotumiwa ili ampatie bibi yake.

Kifo cha mwanafunzi huyo kimetokea juzi wakati akikimbizwa hospitalini baada ya kulalamika kusumbuliwa na tumbo alipokuwa amejifungia chumbani.

Balozi wa nyumba 10 katika mtaa wa Magadula, Tabu Mayenga, alisema baada kupata taarifa ya kifo cha mwanafunzi huyo, alifika msibani kupata chanzo cha kifo cha binti huyo.

Alisema bibi wa wanafunzi huyo aliwaeleza kuwa mjukuu wao alikunywa sumu baada ya kutumia pesa za marejesho ya biashara ya Haice, ambazo babu yake alikuwa akizihitaji na kuamua kunywa sumu.

Hata hivyo, babu wa mwanafunzi huyo, John Hezron ambaye alikuwa akiishi naye aliiambia Nipashe kuwa chanzo cha kifo hicho hakifahamu na hana uhakika kama alikunywa sumu.

Alisema siku ya tukio alikuwa safari jijini Mwanza, alipigiwa simu na mke wake kwamba mjukuu wao analalamika tumbo linamsumbua ndipo akapelekwa hospitali na aliporudi alifika hospitali kumjulia hali na waliruhusiwa na kurudi nyumbani.

Alisimulia kuwa baada ya kurudi nyumbani, muda mchache mjukuu wake alianza tena kulalamika tumbo linamkata na kuamua kumuwahisha tena hospitali, lakini bahati mbaya alifariki dunia wakiwa njiani.

"Mjukuu wangu alikuwa akilalamika tumbo linamkata na hadi umauti unamfika hatujafahamu alikuwa akisumbuliwa na ugonjwa gani, na sisi kama familia hatukuhitaji afanyiwe vipimo zaidi bali kifo chake ni mapenzi ya Mungu na atazikwa kesho (leo)," alisema Kulubone.

"Lakini kunataarifa ambazo zipo mtandaoni kwamba mjukuu wangu amekunywa sumu baada ya kutumiwa hela kwenye simu yake kimakosa, sio kweli, bali yeye alipewa hela za marejesho ya biashara ya Haice na dereva Sh. 61,000, ili ampatie bibi yake, lakini hakufanya hivyo na baadaye akasema pesa zimepotea," alisisitiza.

Aidha, alisema baada ya kukosekana kwa pesa hizo siku hiyo hakulala nyumbani, alienda kwa shangazi yake na aliporudi siku iliyofuata bibi yake alimhoji alikuwa wapi, akamwambia kwa shangazi. Baada ya hapo akaingia chumbani kwake na kujifungia, lakini muda mchache akaanza kulalamika tumbo linamkata hali aliyoendelea nayo hadi umauti ulivyomkuta.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema taarifa za kifo cha mwanafunzi huyo anazisikia juu juu, lakini bado hazijafika rasmi ofisini kwake na kuahidi kuzifuatilia atakaporejea.



Mfugaji akilisha ng'ombe katika Mji wa Mugumu Serengeti, mkoani Mara, mwishoni mwa wiki. Hata hivyo serikali ya wilaya imepiga marufuku mifugo kuchungwa karibu na maeneo ya mji kwa kuwa inachangia uharibifu wa mazingira.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mwili wa kijana aliyesombwa mafuriko wapatikana

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

JESHI la Zimamoto na Uokoaji mkoani Morogoro limefanikiwa kupatikana kwa mwili wa Johnson Moses (16), baada ya kusombwa na maji yaliyosababishwa na mafuriko tangu Januari 11, mwaka huu katika Mto Ulaya, wilayani Kilosa, mkoani hapo.

Kamanda wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, Mrakibu Shabani Marugujo, alisema jana kuwa kijana huyo alisombwa na maji wakati akijaribu kuvuka mto huo na mwili wake kupatikana Januari 13, majira ya saa 12 asubuhi ukiwa unaelea mita kadhaa kutoka alikosombwa pembezoni mwa mto huo.

Kamanda Marugujo alisema mwili wa kijana huyo ulipatikana kutokana na jitihada za kumtafuta zilizofanywa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kushirikiana na wananchi kwa siku tatu.

Alisema elimu dhidi ya tahadhali katika kipindi cha mvua inaendelea kutolewa kwa wananchi wanaoishi maeneo hatarishi kupitia mikutano ya vijiji na vyombo vya habari.

Diwani wa Kata ya Dakawa, wilayani Mvomero, Yusuph Makunja, alisema wakazi wa nyumba 23 zilizobomoka Januari 11 kwa sababu ya mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa iliyonyesha mkoani hapa wanaendelea kukaa kwenye baadhi ya madarasa ya Shule ya Msingi Dakawa.

Alisema mpaka sasa juhudi za kuwatafutia misaada ya chakula na malazi wakazi hao inaendelea kufanywa kwa kushirikiana na uongozi wa wilaya.

## Nyansaho aridhishwa na utendaji wa TANAPA

**Na Maulid Mmbaga**

MJUMBE wa Bodi ya Wadhamini ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Dk. Rhimo Nyansaho, amesema ameridhishwa na utendaji kazi unaofanywa na shirika hilo katika kulinda maliasili na kukuza utalii unaoliongezea taifa mapato.



Dk. Nyansaho aliyasema hayo jana Zanzibar alipotembelea banda la TANAPA katika maonyesho ya 10 ya biashara ya kimataifa, ambako aliwasisitiza watendaji wa shirika hilo kuendelea na juhudi za kuangaza hifadhi za taifa na nyumba ya kumbukizi ya Mwalimu Nyerere iliyopo Dar es Salaam ili iwajengee watoto uzalendo wa kuipenda nchi yao.

Pia alishauri kuwapo na gari maalum la kuwachukua wanafunzi kutoka shuleni na kuwapeleka katika nyumba hiyo ili wafundishwe kuyaishi yale aliyoyafanya kiongozi huyo wakati wa harakati za kupigania uhuru wa Tanganyika.

"Nimeridhishwa na utendaji kazi wa TANAPA kwani juhudi zenu naziona na zimekuwa na matunda chanya ambayo yameendelea kuonyesha tija ya uhifadhi na shughuli za utalii nchini ambazo zinachangia kwa kiasi kikubwa kuliongezea taifa mapato," alisema Dk. Nyansaho.

Naye Ofisa Mwandamizi kutoka Kitengo cha Utalii, Hifadhi ya Taifa Mikumi, Herman Baltazary, alisema lengo la kushiriki katika maonesho ya 10 ya Biashara ya Kimataifa ni katika mwendelezo wa jitihada za kutangaza fursa za uwekezaji zinazopatikana ndani ya hifadhi za taifa.

Aidha, alisema kuwa kutokana na unyeti wa maonyesho hayo pia imekuwa ni fursa nzuri ya kuonana na wadau wa utalii (tour operators), wakala wa usafirishaji na waongoza watalii ili kujenga mahusiano mazuri.

"Mahusiano haya yatasaidia wakati wanapouza fukwe kwa wageni wao wawe na vifurushi pia vya kuvinadi vivutio vya utalii vinavyopatikana ndani ya Hifadhi za Taifa, alisema Baltazary.

MIAKA 60 YA MAPINDUZI

# Majaliwa aguswa maboresho sekta za elimu, afya

**Na Mwandishi Wetu**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiweka jiwe la msingi katika Skuli ya Muungano, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar Januari 10, mwaka huu. **PICHA: OWM**

MAADHIMISHO ya kumbukumbu ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yaliyofanyika Januari 12, 1964 ni muhimu kwa kuwa yanaukumbusha umma wa Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla kuhusu uzalendo uliofanywa na waasisi wa taifa katika kuwatetea wananchi wanyonge.

"Ninafahamu wengi wetu hasa makundi ya vijana hatukuwapo wakati Mapinduzi ya Mwaka 1964 yanafanyika licha ya kuwa ndio tumekuwa wanufaika wakubwa wa mapinduzi yale," alisema Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Jumatano iliyopita baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Skuli ya Muungano iliyoko Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.

Skuli hiyo ambayo itakuwa na madarasa 41, itagharimu Sh. bilioni 6.1 hadi kukamilika kwake. Uwekaji huo wa jiwe la msingi ni sehemu ya shamrashamra za maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Majaliwa alisema kuwa kupitia Mapinduzi ya Mwaka 1964, Zanzibar imeweza kupiga hatua kubwa katika kuwaletea wananchi wote maendeleo bila ya ubaguzi wa aina yoyote kwa kuwa kabla ya Mapinduzi hakukuwa na fursa sawa katika upatikanaji huduma mbalimbali za kijamii, ikiwamo elimu. Alisema awali shule zilikuwa chache na hivyo elimu ilikuwa ikitolewa kwa misingi ya kibaguzi kutegemea na matabaka na jamii kubwa ya Wazanzibar na watoto kutoka familia za kinyonge zilikosa fursa ya kupata elimu, kwa wale wachache waliobahatika, basi walisoma katika shule zenye hadhi za chini kabisa.

"Kwa msingi huo, sina shaka mtakubaliana nami kuwa ilikuwa ni lazima Mapinduzi yafanywe ili kuleta usawa kwa Wazanzibar wote.

"Kama mnavyofahamu, sababu kubwa ya kufanyika Mapinduzi ilikuwa ni kuchoshwa na hali ya ubaguzi mkubwa wa utawala wa kikoloni. Na huu ndio msukumo uliosababisha mwezi Januari 1964, Wazanzibar walishikamana na kuamua kwa pamoja kuuondoa na kujiweka huru na udhalilishaji na madhila waliokuwa wanafanyiwa.

"Wazanzibar walipambana kumwondoa mkoloni kwa kufanya Mapinduzi ambayo leo hii tunajivunia kutimiza miaka 60 kwa kupiga hatua mbalimbali za maendeleo.

"Uhuru tulionao sisi sote katika wakati huu umetokana na ndugu zetu waliojitolea, wakiongozwa na Jemedari wa Mapinduzi Hayati Mzee Abeid Amani Karume, Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi.

"Hivyo basi, sote hatuna budi kuijua vizuri historia hii, kuiheshimu na kutoisahau katika maisha yetu kwa kurithisha vizazi na vizazi, kuilinda na kutorudi nyuma," alihimiza.

**SEKTA YA ELIMU**

Waziri Mkuu alisema historia ya mageuzi katika sekta ya elimu ilianza tarehe 23 Septemba 1964, ambapo Serikali ya Mapinduzi iliyoongozwa na Hayati Mzee Abeid Aman Karume, ilitangaza elimu bure kwa wananchi wote bila kujali rangi, kabila, dini, eneo wanalotoka au hata jinsia, mpango wa elimu bure umeendelea kudumishwa katika awamu zote za uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi sasa wanapoadhimisha miaka 60 tangu kufanyika Mapinduzi hayo.

Majaliwa alitumia fursa hiyo kueleza baadhi ya mafanikio yaliyopatikana upande wa sekta ya elimu katika kipindi cha miaka 60 ya Mapinduzi kuwa pamoja na kuwapo wa vyuo saba vinavyotoa masomo ya ngazi ya elimu ya juu ambapo kabla ya Mapinduzi hakukuwa na chuo kikuu hata kimoja.

Alisema vijana mbalimbali wanaomaliza masomo yao ya sekondari, sasa wanapata fursa ya kujiunga na masomo ya vyuo vikuu ndani na nje ya Tanzania, ambapo katika kipindi hiki, idadi ya wanafunzi waliosajiliwa katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) pekee imefikia wanafunzi 7,250 kwa mwaka 2023 kutoka wanafunzi 53 mwaka 2000 kilipoanzishwa.

Majaliwa pia alisema serikali imefanikisha kuanzisha Tawi la Chuo cha Teknolojia, Institute of Technology Madrsa (IITM) cha India ambacho ndio chuo cha kwanza kwa ubora India.

"Kuwapo chuo hiki kunaifanya Zanzibar kuwa nchi ya kwanza barani Afrika kuwa na tawi la chuo hicho na hivyo kutoa fursa kubwa kuitangaza Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kimataifa," alisema.

Waziri Mkuu alisema uanzishwaji chuo hicho ni katika hatua ya utekelezaji Dira ya Maendelo ya Zanzibar ya 2050 inayoelekeza kuimarisha ujuzi na utaalamu kwa wananchi katika kufikia uchumi na jamii iliyo bora na chuo hicho kitatoa wataalamu waliobobea kwenye masuala ya teknolojia na hivyo kuwa chachu ya utatuzi wa changamoto zinazolikabili taifa katika sekta mbalimbali kama vile nishati, kilimo, afya, elimu na viwanda.

"Kama mlivyosikia hapo awali, fursa za upatikanaji elimu zilikuwa chache katika ngazi zote, lakini kutokana na jitihada kubwa zinazoendelea kufanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mageuzi makubwa yamefanyika katika kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kuongeza miundombinu ya elimu, ambapo sasa serikali imeanza utekelezaji mradi wa ujenzi wa vyuo vitano vya kisasa vya mafunzo ya amali kote nchini," alibainisha.

Majaliwa alisema ujenzi wa vyuo hivyo utakamilisha shabaha ya serikali kuwa na chuo cha amali kikubwa na cha kisasa katika kila wilaya kwa lengo la kuhakikisha vijana wanapata ujuzi na utaalamu utakaowasaidia kukabiliana na ushindani wa soko la ajira ndani na nje ya nchi hasa katika fani za uchumi wa buluu.

Vilevile, kupitia mradi huo, serikali itajenga na kukipatia vifaa Chuo cha Ubaharia na kutanua Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ili kuongeza fani mbalimbali zinazotolewa na chuo hicho zikiwamo mafuta na gesi.

"Serikali pia inajenga ofisi za elimu za wilaya na kuzipatia vifaa ambapo mbili tayari zimeshafunguliwa katika sherehe hizi zinazoendelea za maadhimisho ya kutimiza Miaka 60 ya Mapinduzi.

"Ujenzi wa ofisi hizi utaimarisha ufuatiliaji na usimamizi katika utoaji na upatikanaji elimu bora. Kuziunganisha skuli zote na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kufundishia na kujifunzia," alisema.

**SEKTA YA AFYA**

Waziri Mkuu pia alisema Rais Dk. Mwinyi amedhamiria kuimarisha miundombinu ya sekta ya afya ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma katika mazingira bora na kwa viwango vinavyokubalika ikiwa ni pamoja na kuendelea kuweka mifumo imara ikiwamo mfumo wa rufani utakaozingatia huduma bora zinazotolewa kwa wakati.

Alisema miradi ya ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya inatekelezwa ili kusogeza huduma bora karibu na wananchi, kupunguza msongamano na kufanya utoaji huduma za afya uwe rafiki kwa watoa huduma na kwa wananchi.

Alisema ujenzi wa vituo vya kisasa vya kutolea huduma za afya utapunguza gharama kwa kuwa kwa muda mrefu serikali imekuwa inatumia fedha nyingi kugharamia matibabu ya wananchi nje ya nchi.

"Serikali imeanza na itaendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya ili madaktari bingwa na bobezi wazalendo na wale wa kigeni waweze kuwa na mazingira rafiki ya kutoa huduma za kibingwa na kibobezi katika hospitali zetu za kisasa zilizopo nchini," alisema.

Waziri Mkuu alisema kutokana na jitihada hizo, serikali imeshajenga hospitali 10 za wilaya katika wilaya za Unguja na Pemba, na kila hospitali ina vifaa tiba kamili na magari ya kisasa ya kubebea wagonjwa kwa ajili ya kutoa tiba stahiki za dharura na rufani.

"Hospitali hizo zote ni nzuri na zina huduma zote za kisasa kama lilivyo jengo hili la Hospitali ya Wilaya ya Kaskazini B.

"Mradi huu wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kaskazini B ni matokeo ya mipango thabiti na utekelezaji ahadi ya serikali yetu tukufu zinazokwenda sambamba na utekelezaji mikakati ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964. Serikali iliahidi itatekeleza na leo tumefungua hospitali hii mpya ambayo ina hadhi ya wilaya na itatoa huduma za afya kwa mfumo wa kidijitali," alisema.

**WAZIRI WA AFYA**

Waziri wa Afya Zanzibar, Nassoro Ahmed Mazrui, alisema takwimu zinaonesha Zanzibar kuna mapinduzi makubwa ya huduma za afya katika sekta ya umma kwa kuwa wametoka kuwa na vitanda 1,445 vya kulaza wagonjwa na sasa vipo takribani vitanda 2,645 vya kulaza wagonjwa katika hospitali za Unguja na Pemba.

Alisema awali kulikuwa na chumba kimoja tu kwa ajili ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU) katika Hospitali ya Rufani Mnazimmoja chenye vitanda vinane na sasa hivi kuna jumla ya ICU 14 na vitanda 80 vya ICU ikiwa ni pamoja na vitanda sita vya ICU vilivyokuwamo ndani Hospitali ya Wilaya ya Magharibi A.

Waziri huyo pia alisema kulikuwa na vyumba vya upasuaji 11 na kati yake viwili ni maalum kwa ajili ya kinamama wenye mahitaji ya kujifungua kwa upasuaji na sasa hivi kuna vyumba 35 vya upasuaji vikiwamo 13 maalum kwa ajili ya kinamama na vitengo vya dharura vimeongezeka kutoka viwili hadi 13.

**WAZIRI WA ELIMU**

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, alitumia fursa hiyo kutaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya elimu katika kipindi cha miaka 60 ya Mapinduzi kuwa ni pamoja kuongezwa bajeti ya sekta ya elimu kutoka Sh. bilioni 265.5 mwaka 2021/22 hadi kufikia Sh. bilioni 457.2 mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 72.2.

Alisema kiwango hicho cha bajeti katika historia ya Zanzibar ni kielelezo cha dhamira ya serikali katika kuendeleza sekta ya elimu, ambapo kwa sasa imejipanga kujenga shule 25 za ghorofa katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba kwa mwaka wa fedha wa 2023/24; ikiwamo shule hiyo ya ghorofa tatu (G+3) ya Muungano.

Alisema mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya shule zinazotoa elimu ya maandalizi kutoka shule moja tu mwaka 1964 hadi kufikia skuli 891 mwaka 2023.

Vilevile, waziri huyo alisema kuwa katika kipindi hicho shule zinazotoa elimu ya msingi zimeongezeka kutoka 62 hadi 649, shule za sekondari zimeongezeka kutoka tano na kufikia shule 318 mwaka 2023.

"Uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi zote za elimu (Maandalizi, Msingi na Sekondari) umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka wanafunzi 25,432 mwaka 1964 na kufikia wanafunzi 592,781 mwaka 2023.

"Ukuaji huu wa uandikishaji wanafunzi umetokana si tu kwa sababu ya ongezeko la idadi ya watu, bali pia elimu kuwa ni haki ya msingi kwa kila mtoto.



# Polisi yapiga kambi kwa wafugaji

**Na Allan Isack,** MONDULI

JESHI la Polisi limeanzisha kampeni ya kukabiliana na matukio ya uhalifu na ukatili wa kijinsia kwa jamii za wafugaji wilayani hapa Mkoa wa Arusha.

Kampeni hiyo inafanywa na wakaguzi wa jeshi hilo wa ngazi ya kata kwa kuwafuata wazee wa mila na makundi rika kuzungumza nao na kuwapa elimu ya namna ya kukataa vitendo hivyo kuendelea kukithiri katika jamii yao.

Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Juma Mahega anayehudumu Kata ya Selela alisema hatua hiyo ni moja ya kampeni ya kuziwezesha familia hasa watoto kuanza kufahamu uhalifu na namna ya kukabiliana nao mapema.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi na viongozi wa kijiji hicho walisema hatua hiyo itasaidia kujenga kizazi kitakachokuwa kinachukia uhalifu kijijini hapo.

Neema Mollel, Mkazi wa kijiji hicho alisema matukio ya uhalifu yamepungua kwa kiasi kikubwa tangu mkaguzi huyo aweke kambi kijijini hapo.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Selela, Neema Daud alisema kitendo cha kuwaelimisha watoto kinachofanywa na Jeshi la Polisi kupitia mkaguzi huyo kitaleta tija kwa baadaye.

"Amekuwa ni mtu mwenye ushirikiano mkubwa kati yetu na wananchi, kampeni hizi za kutoa elimu kwa jamii zimeanza kuleta mabadiliko baada ya vijana wengi kuanza kushirikiana vema na Jeshi la Polisi na mamlaka nyingine za kiusalama," alisema Ofisa Mtendaji huyo.

**Neema Mollel, Mkazi wa kijiji hicho alisema matukio ya uhalifu yamepungua kwa kiasi kikubwa tangu mkaguzi huyo aweke kambi kijijini hapo.**

# Hospitali ya Bombo yapokea waraibu watatu kwa siku

**Na Oscar Assenga,** TANGA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo) kwa siku inapokea waraibu wawili hadi watatu wa dawa za kulevya walioathiriwa na ugoro, mirungi, bangi na uvutaji petroli.

Kwa mujibu wa Daktari wa Magonjwa ya Afya ya Akili wa hospitali hiyo, Wallace Karata hadi kufikia Januari 10, mwaka huu, waraibu 28 walikuwa wamekamilisha matibabu yao.

"Kwa sasa kwa wiki moja tunapokea idadi ya waathirika wa dawa za kulevya 12 mpaka 13.

Mwitikio wa waraibu kujitokeza ili kupata matibabu, unatokana na asasi za kiraia kuwaibua kutoka kwenye vijiwe, fukwe na maeneo wanayopatikana wakiwa wanafanya matumizi ya dawa hizo," alisema Dk. Katara.

Dk.Karata alisema jana kuwa Wizara ya Afya na wadau wamewezesha upatikanaji wa vifaa kazi ambavyo vitawasaidia waraibu hao kujikwamua kiuchumi.

Alisema kwa sasa kituo hicho kina mashine za kutengeneza tofali, kuosha magari, kushona nguo na vifaa vya saluni.

Daktari huyo aliongeza kuwa waraibu hao, watakuwa wanawaandalia zaidi miradi ya ujasiriamali baada ya kupata nafuu.

"Jambo hili ni hatua kubwa sana na yakupongezwa kwani changamoto iliyopo kwenye jamii ni ukosefu wa shughuli za kufanya baada ya kupata nafuu, lakini mpango huo utakuwa chachu yao kushiriki shughuli za kiuchumi na hatimaye kupata maendeleo," alisema

**"Kwa sasa kwa wiki moja tunapokea idadi ya waathirika wa dawa za kulevya 12 mpaka 13.**



Mfanyabiashara wa matunda katika Soko Kuu karibu na Msikiti wa Ijumaa wilayani Muheza, Tanga, Athuman Mahea (kushoto), akisubiria wateja ili kuwauzia mafenesi juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kijazi kujitosa kutangaza utalii nchini

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KAMISHNA wa zamani wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Dk.Allan Kijazi ametangaza mpango wake wa kufungua kampuni ya kutoa ushauri katika masuala ya utalii na uhifadhi wa ardhi nchini.

Akizungumza na Nipashe jana jijini hapa, Dk.Kijazi, alisema baada ya kustaafu na kupumzika kwa mwaka mmoja, anajiandaa kufungua kampuni hiyo.

"Lengo langu niendelee kutumia ujuzi wangu nilionao katika maeneo haya ili niendelee kusaidia kutatua changamoto zinazojitokeza kwenye maeneo haya na kuleta mafanikio kwa nchi yangu," alisema na kufafanua kuwa:

"Ndoto hii imekuja baada ya watu wengi kunifuata wakiniomba ushauri kwenye maeneo haya nikaona bora niwe na kampuni."

Awali alivishauri vyombo vya habari nchini kuendelea kuhamasisha Watanzania kutembelea hifadhi nchini ili kukuza utalii wa ndani.

Dk.Kijazi ambaye pia ni Katibu Mkuu Mstaafu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alisema utalii wa ndani una umuhimu mkubwa kuliko kutegemea watalii wa nje ya nchi pekee.

"Katika hili naona bado kuna umuhimu wa vyombo vya habari nchini kuongeza nguvu ya uhamasishaji wa utalii huu ili tuongeze kiwango cha watalii wa ndani kwenye hifadhi zetu," alisema.

Alisema ili vyombo vya habari vihamasishe zaidi umuhimu utalii huo ni vizuri wakapatiwa elimu zaidi juu ya masuala ya uhifadhi.


"Nasema hivi kwa sababu vipo vyombo vya habari havijui kutofautisha kati ya maeneo ya hifadhi uwindaji na mapori ya akiba, hivi vitu vinawachanganya, hivyo vema wakapatiwa elimu hizo mara kwa mara ili wafanye kazi yao kiweledi zaidi," alisema.

Alishauri wadau wa utalii kwa kushirikiana na serikali watafutiwe usafiri wa kudumu wa kupeleka Watanzania kwenye hifadhi kwa bei rafiki.

Pia zifanyike jitihada ya kujenga malazi ya bei nafuu maeneo ya hifadhi ili kuwezesha wananchi kumudu wanapotembelea vivutio.

"Wapo baadhi ya Watanzania wanatamani kutembelea hifadhi wanashindwa sababu ya bei kubwa za usafiri na malazi, tukiboresha haya yote utalii wa ndani utaongezeka maradufu na kuleta tija kwenye pato la Taifa," alisema.

Alisema serikali imejitahidi kujali wazawa kwa kuweka kiingilio rafiki kwenye hifadhi ili kuwezesha wananchi kutembelea vivutio.



# Chemba vyoo MWAUWASA zazua hofu kwa wananchi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya wakazi wa Jiji la Mwanza wameiomba Serikali kurekebisha mifumo ya maji taka ili kudhibiti kuzuka kwa kipindupindu kutokana na uchafu kusambaa kwenye makazi yao.

Mkazi wa Mtaa wa Magomeni wiliayani Ilemela, Theonest Theodory alisema kuwa kuna chemba za vyoo zinarudisha majitaka kwenye makazi yao na kusababisha hofu miongoni mwao ya kukumbwa na kipindupindu.

"Tunalipa bili za majitaka na majisafi, kwa zaidi ya miaka miwili sasa miundombinu ya majitaka ni mibovu na haifanyi kazi, kama hawawezi waje watufanyie tathimini waturudishie fedha zetu za maji taka," alisema Theodory.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Magomeni Abdallah Hega alisema ameandika barua kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kulalamikia tatizo hilo.

Hega alisema baada ya kupokea barua hiyo waliahidi kuwa wangefika kwenye maeneo yao na kurekebisha kwa kufunga mashine nyingine mpya, lakini mpaka sasa hawajafanya hivyo.

Akizungumza na Nipashe Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira MWAUWASA, Salim Lossindilo alisema Mamlaka hiyo imesaini mkataba Novemba 23, mwaka juzi wenye thamani ya Sh.bilioni 12.7 kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya maji taka katika maeneo ya Ilemela na Jiji la Mwanza.

"Kwa sasa kazi ya kuhuisha usanifu wa mradi inaendelea na itakapokamilika taratibu za manunuzi ya mkandarasi zitafanyika ikiwa matarajio ni kuanza kazi za ujenzi mapema mwaka huu na kukamilika Mwaka 2026," alisema na kusisitiza kuwa: "Baada ya kukamilika tuna imani kuwa tatizo hili litakuwa limedhibitiwa kwa asilimia 100."



Taka zilizosombwa na maji kutoka maeneo mbalimbali ya milimani wakati wa mvua kupitia Mto Milongo zikiwa zimekwama baada ya mvua kuacha kunyesha katika eneo la Mlango Mmoja. **PICHA: REMY MOKA (SAUT)**

## Mabilioni ya maendeleo yapokewa Sikonge

**Na Halima Ikunji,** SIKONGE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora imepokea Shilingi bilioni 10 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya elimu, barabara, maji na afya kwa ajili ya wananchi.

Kaimu Mkurungezi wa Halmashauri hiyo, Nico Kayange aliyasema hayo juzi ofisini kwake wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo.

"Hatutakubali kuona miradi inashindwa kumalizika kisa kuna baadhi ya viongozi wametafuna fedha za umma, sheria itachukua mkondo wake," alisema Nico.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2023/2024, halmashauri hiyo ilipokea Shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya elimu ili kuondoa adha kwa wanafunzi kutembea umbali mrefu na kusogeza huduma za afya karibu na wahitaji, wakiwemo wajawazito na watoto.

Alisema Shilingi milioni 250 zilitumika kujenga jengo la mionzi, nyumba za watumishi na umaliziaji wa jengo la kufulia nguo katika Kituo cha Afya Tutuo. Nico alisema fedha hizo pia zilisaidia kutoa huduma za afya, lishe na ustawi wa jamii kwa watoto wanaopata huduma kwenye kituo hicho cha afya Tutuo.

Kwa mujibu wa Nico, kiasi cha Shilingi milioni 300 zilitumika kununulia vifaa tiba katika jengo la dharura la Hospitali ya Wilaya ya Sikonge.

Alisisitiza kuwa fedha hizo zilifanya kazi kubwa kuboresha miondombinu ya shule za msingi na sekondari, kujengwa shule mpya ya sekondari Sikonge kwa Shilingi milioni 603.8.

# Jiji lalamikiwa kwa kutelekeza dampo

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

HALMASHAURI ya Jiji la Mwanza imelalamikiwa kwa kutelekeza takataka kwenye dampo lililopo kwenye eneo kilipokua kituo cha mabasi kwa zaidi ya miezi miwili.

Mkazi wa Mtaa wa Nyaburogoya, Salvatory Mgalula alidai kuwa kitendo cha halmashauri hiyo kutelekeza takataka hizo kwenye eneo hilo kimesababisha harufu mbaya kwenye maeneo hayo na kuwepo kwa tishio la kuzuka kipindupindu.

"Huu ulikuwa uwanja wa shule na hakukuwa na dampo, lakini baada ya kuweka stendi hapa kwa muda wakaweka na dampo hili na vifaa vya kukusanya taka baada ya siku makontena wameyaondoa na taka zimeachwa hapa wakati wa mvua kama sasa hali inakuwa mbaya zaidi," alisema Mgalula

Ofisa Afya na Mazingira Jiji la Mwanza, Desderius Polle alithibitisha kuwepo kwa taka katika eneo hilo na jukumu la kuziondoa ni la halmashauri hiyo.

Polle alisema utaratibu wa kuondoa taka hizo unaendelea kwa ratiba na pindi zitakapoisha eneo hilo litabadilishiwa matumizi.

"Yapo maeneo tofauti tunayohudumia likiwemo hilo ambalo lilikuwa eneo la kituo cha mabasi cha muda Nyegezi, lakini baada ya stendi kukamilika uzalishaji taka umepungua hivyo tunaendelea kuziondoa kwa awamu na zitakapoisha eneo hilo tunalifanya la nyama choma kwa jiji letu," alisema Polle.

Mwanza umekuwa miongoni mwa mikoa iliyotajwa kukumbwa na kipindupindu nchini baada ya zaidi ya watu 30 kudaiwa kukutwa na vimelea vya ugonjwa huo, huku mmoja akithibitika kufa.

Hali hiyo ilimlazimu Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla kuagiza maeneo yote ya afya kutoa tiba bure kwa wagonjwa wa kipindupindu.

Vilevile, Mongela aliagiza mamlaka za barabara mkoani hapa kuhakikisha mifereji inazibuliwa ili maji yasituame.

Kwa upande wa mamlaka za maji, aliziagiza kuhakikisha maji yanatibiwa kabla ya kumfikia mlaji.



Ukurasa 12

**Ujio somo la amali, wadau waibua mbinu kulipa matokeo chanya**



Ukurasa 13

Udanganyifu na matusi mitihani unavyosadifu ukosefu maadili

Nipashe TESA

Jumanne Januari 16, 2024

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Usahaulifu, unene kupindukia magonjwa pasua kichwa yanayoelekea kukomeshwa**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Wajawazito wanapotumia dawa kwa njia hizi, wanajiangamiza na watoto wao

ZIPO hisia kuwa zama hizi zina watoto wengi wenye hitilafu kimaumbile, pengine wana ulemavu wa akili, usonzi na baadhi wamelemaa viungo.

Jamii inataja sababu nyingi kama, wajawazito kutumia vilevi, vinywaji vya kuongeza nguvu na pia ikigusia matumizi ya vikinga mimba vinavyotolewa kwenye uzazi wa mpango.

Lakini lipo jambo jingine, kutumia dawa zikiwamo antibayotiki bila maelekezo ya daktari. Wapo wajawazito ambao huwatuma waume au jamaa zao wa karibu kuwanunulia dawa, lakini wanapofika dukani, hawaelezi kuwa wametumiwa na wajawazito, huchukua dawa na kuwapelekea hilo nalo lina athari.



Mjamzito akijitunza amemtunza na mwanawe pia. **PICHA: MTANDAO**

Mteknolojia wa dawa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga Deogratius Ngofongo, anataja baadhi ya dawa ambazo ni hatari kwa wajawazito akianza na Asprin, ambayo ni hatari sababu hufanya kazi kama damu imeganda ili kuilainisha.

Iwapo mjamzito ameitumia sana, kipindi cha kujifungua damu zinaweza kutoka kwa wingi na hata kupoteza maisha yake na mtoto.

Anataja dawa nyingine kuwa ni Ciprofloxacin, ambayo ni hatari hasa ujauzito unapokuwa na miezi mitatu, akisema inapita kwenye mfuko wa uzazi na kuleta madhara makubwa kwa mtoto.

"Dawa yoyote ni sumu ukiitumia bila maelekezo ya daktari inaweza kukuletea madhara makubwa mwilini, ushauri kwa wajawazito wasitumie dawa yoyote kabla ya kupata vipimo kutoka kwa wataalamu wa afya na kuelekezwa dawa sahihi ya kutumia ili kumlinda mtoto tumboni," anasema Ngofongo.

Anaongeza: "Mjamzito akitumia dawa kiholela zina madhara makubwa katika ukuaji wa mtoto na wakati mwingine mimba inaweza kuharibika na kuua mtoto, nawasihi wajawazito wapende kuhudhuria kliniki kipindi cha ujauzito ili wapate ushauri wa wataalamu kwenye matumizi sahihi ya dawa, wasijiamulie dawa za kumeza," anaongeza Ngofongo.

Wataalamu wa afya wanasisitiza kuwa unapokuwa mjamzito unapaswa kuwa na uangalifu zaidi ili kuepuka kujiingiza kwenye mambo yanayoweza kuhatarisha hatima ya mtoto wake ambaye hajazaliwa.

Mathalani, kupata elimu ya matumizi sahihi ya dawa ambazo huthibitishwa na daktari ili kusaidia ukuaji wa mtoto tumboni kadhalika kuzua asiathiriwe na matumizi holela ya dawa na mimba kuharibika.

Mjamzito anapomeza dawa ni lazima kuwa zitamfikia mtoto kupitia michakato ya kumeng'enya na kufyonza chakula, iwapo ametumia dawa ambazo siyo sahihi au hazijathibitishwa na daktari, zinaweza kuleta madhara katika maendeleo ya ukuaji wa mtoto tumboni.

### MADHARA YA DAWA

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, dawa nyingi huleta madhara hasa ujauzito unapofikisha miezi mitatu sababu ni kipindi ambacho viungo mbalimbali vya mtoto huanza kutengenezwa, hivyo matumizi holela ya dawa huathiri uumbaji wake.

Madhara ambayo humpata mtoto kutokana na matumizi holela ya dawa ni kutokua ipasavyo, kupata maumbile yasiyo ya kawaida, kudumaa kabla ya kuzaliwa, mama kujifungua kabla ya wakati akiwa njiti, kupata utindio wa ubongo na kufariki akiwa bado tumboni au mimba kuharibika.

### ELIMU MATUMIZI

Ofisa Muuguzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga Daniel Magina, anasema wajawazito ambao hufika kwenye hospitali hiyo hupatiwa elimu ya matumizi sahihi ya dawa, kipindi chote cha ujauzito hadi kujifungua.

Anasema anayehudhuria kliniki hawezi kutumia dawa holela, sababu hupimwa na kuelekezwa dawa anazopaswa kuzitumia kutokana na hatua ya ujauzito wake au tatizo ambalo lina msumbua, lakini wale ambao hawahudhurii ndiyo hukumbwa na matatizo na madhara ya kutumia dawa ovyo.

Mjamzito Hadija Mustapha, anatarajia kujifungua wakati wowote katika hospitali hiyo ya rufani mkoani Shinyanga, anasema hawezi kunywa dawa bila maelekezo ya daktari, baada ya kuelezwa kuwa ni hatari mjamzito kutumia dawa kiholela.

Anasema ni elimu aliyoipata hospitalini siku ya kwanza alipohudhuria kliniki, na sasa amefika akitarajia kujifungua.

Stella Manumbu, anasema tatizo la wajawazito kutumia dawa kiholela lipo hasa katika maeneo ya vijijini, ambapo wengi wao hawana elimu kutokana na huduma za afya kuwa mbali na wananchi na hivyo kwenda kwenye maduka ya dawa yaliyo jirani na kuomba ushauri na kununua dawa pia.

Anasema wanafanya hivyo baada ya kusikia maumivu au kuona hali fulani na lakini wakizitumia bila ya kujua madhara na athari zake.

"Vijijini mjamzito anaweza kujisikia vibaya akamtuma mumewe au mtu aliye karibu naye kwenye duka la dawa amnunulie dawa ya maumivu. Mteja akifika anaomba dawa ya maumivu muuzaji anampatia bila kueleza kuwa anampelekea mjamzito.Akiletewa anameza mwishoni anapata matatizo,"anasema Stella.

INAENDELEA UK.14

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Ujio somo la amali, wadau waibua mbinu kulipa matokeo chanya




Wahitimu wa mafunzo ya amali wakiunda mitambo baada ya kujifunza ufundi. **PICHA: SIDO**

MABORESHO mengi yamefanyika kwa mitaala, ambayo yanakwenda kubadilisha mfumo mzima wa elimu, miongoni mwake ikiwa ni sekondari kuwa na mikondo miwili, wa jumla na amali (ufundi), huku mwanafunzi akichagua kutokana na uwezo na malengo yake ya baadaye.

Mkondo wa ufundi utakuwa na fani za kilimo, ufugaji, umakanika, biashara, ujasiriamali, sanaa, ubunifu, elimu ya michezo, ufugaji nyuki, uchimbaji wa madini na mambo ya urembo.

Aidha, mwanafunzi wa mkondo wa ufundi atatakiwa kuchukua masomo manne ya jumla na moja la fani ambayo ni hisabati, elimu ya biashara, Kiingereza, Historia ya Tanzania na maadili.

Aidha, wahitimu wa ufundi watapata vyeti viwili, kikiwamo cha ujumla cha elimu ya sekondari (NECTA) na cheti cha amali (NACTIVET), na pia kila shule itakuwa na wakala wa VETA, ili kusimamia ufundi.

Maboresho hayo, ambayo lengo lake ni mwanafunzi kuhitimu akiwa tayari ana ujuzi, kwa ajili ya kujiari au kuajiriwa, yanakuja wakati serikali ikiwa na mkakati wa kujenga vyuo vya ufundi kila wilaya.

> “Labda kwenye maboresho haya ya elimu hasa katika somo la amali, kutakuwa na vifaa vya kutosha vya kufundishia kila somo?

Kutokana na mazingira hayo, Nipashe inazungumza na wadau wa elimu kupata maoni yao kama kuna haja ya kuendelea kujenga vyuo hivyo kila wilaya wakati elimu ya ufundi ikitolewa shuleni.

Dk. Anna Henga ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ambaye anasema hana shaka na kuwapo VETA kila wilaya, ila hana uhakika kama elimu hiyo itatolewa kwa vitendo.

“Unapozungumzia suala la ufundi au ufugaji ikiwamo wa nyuki, ni kujifunza kwa vitendo siyo wanafunzi kuchorewa mizinga ubaoni badala ya kwenda maeneo ya kufugia nyuki na kujifunza,” anasema Dk. Anna.

Mkurugenzi Mtendaji huyo anasema, elimu ya ufundi inahitaji bajeti ya kutosha ili wanafunzi wajifunze kwa vitendo, na wanapohitimu waweze kuendeleza ujuzi huo kwa maisha yao ya baadaye.

“Kwahiyo, ili elimu ya amali iwe na manufaa kwa wanafunzi, ni vyema wanafunzi wajifunze kwa vitendo na ili wajifunze kwa vitendo, ni serikali kutenga fedha za kutosha za kununulia vifaa husika,” anasema.

Kuhusu mkakati wa serikali wa kujenga VETA kila wilaya, anasema, serikali iendelee kujenga vyuo hivyo, kwa kuwa vinasaidia hata watu wengine ambao si wanafunzi kupata elimu ya ufundi.

Anasema vyuo vya VETA si kwa wanafunzi tu bali kila anayehitaji kupata elimu ya ufundi anaruhusiwa na kwamba inawezekana hata hao watakaopata elimu ya amali wakahitaji kwenda katika vyuo hivyo.

“Kama serikali itakuwa haijajipanga vizuri, kuna uwezekano wanafunzi wa elimu ya amali wakapata elimu bila vitendo na hivyo kujikuta wakienda VETA baada ya kuhitimu elimu yao,” anasema.

Meshack Kapange, Katibu Mkuu wa Chama Cha Kutetea Haki Na Maslahi Ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA), anasema kuna uwezekano wa wanafunzi kufundishwa bila vitendo.

Anasema uzoefu unaonyesha kuwa kumekuwa na ugumu kufundisha masomo kwa vitendo, sababu kuu ikiwa ni ukosefu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

“Kwa mfano somo la TEHAMA, shule nyingi zimekuwa zikifundisha kwa nadharia na kusababisha wanafunzi kutoelewa vizuri somo hilo, hilo ninaona linaweza kutokea kwenye elimu hii,” anasema Kapange.

Anafafanua kuwa shule nyingi hazina kompyuta, hatua inayosababisha wanafunzi kushindwa kujifunza somo la TEHAMA kwa vitendo, na kwamba mazingira hayo yanaweza kuwapo hata katika somo la amali.

“Ninadhani maboresho haya ya mitaala ya elimu yanaweza yasiwe na tija sana, halafu wanasema kila shule itakuwa na wakala wa VETA, hivi vyuo hivyo vina watumishi wangapi wa kuenea shue zilizopo,” anasema.

Aidha, anasema suala la serikali kujenga VETA kila wilaya ni zuri, lakini anahoji kama kuna watalaam wa kutosha? Lakini pia anafafanua kuwa huenda vikasaidia wanafunzi wa elimu ya amali, kwa maelezo kuwa hana uhakika kama wanafunzi wa sekondari watajifunza kwa vitendo.

Mkurugenzi wa kampuni inayojishughulisha na masuala ya ubunifu ya Sahara Venture, Musa Kamata anasema, kuwapo kwa VETA kila wilaya hakuna uhusiano na mafunzo ya ufundi shuleni.

“Ninachojua, kila mwanafunzi atachagua mkondo anaoutaka, wapo watachukua ufundi na wengine hawatakwenda huko, lakini ikumbukwe kuwa VETA si kwa ajili ya wanafunzi tu,” anasema Kamata.


Anasema serikali inajenga VETA kila wilaya kwa ajili ya Watanzania wote ambao wanahitaji kupata ujuzi, kwamba isichukuliwe kuwa ni kwa ajili ya wanafunzi wanaohitimu sekondari tu.

“Labda kwenye maboresho haya ya elimu hasa katika somo la amali, kutakuwa na vifaa vya kutosha vya kufundishia kila somo? Umakanika unahitaji spana na vifaa vingine vinavyohusina na ufundi,” anasema.

Anafafanua kuwa uwe ufugaji nyuki, kilimo, ujasiriamali, ubunifu, vyote vinahitaji vitu vya kufundishi, na kwamba serikali haina budi kujipanga kufundisha masomo hayo kwa vitendo.

ELIMU
NA DK. REUBENI LUMBAGALA

# Udanganyifu na matusi mitihani unavyosadifu ukosefu maadili



WANAFUNZI kuanzia shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vikuu hupata maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali kwenye taasisi za elimu wanazosoma.

Katika kufanikisha kufundisha na kujifunza shuleni au vyuoni, walimu wanawajibika kufundisha huku wanafunzi wakitakiwa kusikiliza na kuzingatia elimu wanayopewa ili kutimiza malengo hasa kuvuka na kuendelea na ngazi za juu zaidi.

Tamati ya kujifunza huhitimishwa na kupima wanafunzi yale waliyofunzwa, kazi inayofanyika kwa mfumo wa kutoa mazoezi, majaribio na mitihani ikiwamo upimaji kitaifa.

Kupima uelewa hutoa taswira ya jinsi wanafunzi katika kipindi fulani cha ujifunzaji walivyoelewa mambo. Mathalani; upimaji kitaifa darasa la nne, huleta picha ya kuelewa kwa namna gani au kiwango wanafunzi katika yale waliyojifunza miaka minne kuanzia la kwanza hadi la nne.

Kwa wanafunzi wa darasa la saba, hupimwa katika yale waliyojifunza katika kipindi cha miaka saba, kadhalika mtihani wa kitaifa kidato cha pili hupima wanafunzi katika yale waliyojifunza kwa miaka miwili, hali kadhalika kidato cha nne hujumlisha uelewa wa miaka minne darasani na ule wa miaka miwili ya elimu ya kidato cha sita unapimwa kwenye mtihani wa kidato hicho.

Ili wanafunzi wafanye vyema katika mitihani hiyo, walimu wanawaandaa kikamilifu kwa kuwafundisha ipasavyo huku nao wakiwajibika kujisomea vya kutosha ili kujibu vyema mitihani hiyo na kuendelea na ngazi nyingine kimasomo.

### KUIBUKA UDANGANYIFU

Baadhi ya watu wasiolitakia mema taifa lao, hufanya hujuma au udanganyifu kwenye mitihani ili watoto au wanafunzi wao wafanye maajabu kwa kuibuka na alama A.

Udanganyifu umekuwa na madhara kwa watahiniwa wenyewe, kwa shule wanazosoma na taifa kwani unasababisha kufutiwa matokeo, shule kufutiwa usajili na nchi kupata hasara ya kuandaa mitihani kwa gharama zaidi lakini kuzalisha wasomi wasio na sifa stahiki.

Hivyo kuhatarisha ustawi wa ujuzi na maendeleo kwa kuwa wasomi hawana ujuzi wala hawafahamu mambo.

Baadhi ya watahiniwa huandika matusi kwenye mitihani ya kitaifa, jambo hili ni hasara kwenye ujenzi wa taifa lenye wanafunzi wanaosomeshwa elimu ikigharamiwa na serikali, wazazi na walezi.

Ni kwa sababu watahiniwa hawa ni sehemu ya raia wanaotakiwa kutoa majibu sahihi na si matusi, ambayo ni tabia mbaya isiyokubalika kuanzia kwenye imani za dini hadi kwenye tamaduni ndani ya jamii.

Hata katika uga wa kisheria, matusi ni kosa la jinai, hivyo haikubaliki na pengine wanaofanya hayo wanastahili kuadhibiwa siyo kwa maonyo shuleni.

Akitangaza matokeo ya kitaifa ya upimaji wa darasa la nne na kidato cha pili, Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), Dk. Said Mohamed anasema baraza limefuta matokeo kwa watahiniwa 206, kati yao wanafunzi 178 wa darasa la nne na 28 wa kidato cha pili kwa kufanya udanganyifu.

Vilevile, NECTA imewafutia matokeo watahiniwa 17, watatu wa darasa la nne na 14 wa kidato cha pili walioandika matusi kwenye karatasi za kujibia mitihani yao.

Pamoja na sababu kadhaa ambazo wataalamu wanaweza kuja nazo kama chanzo cha udanganyifu na uandishi wa matusi kwenye mitihani, lakini kubwa ninaloliona hapa ni mmomonyoko wa maadili.

Katika suala la udanganyifu kwenye mitihani, ni muhimu wazazi, walezi, walimu na wanafunzi wenyewe kuzingatia maadili.

Kudanganya mitihani ni zao la mmomonyoko wa maadili kwani kwa wazazi, walezi, walimu na wanafunzi wenye maadili mema hawatakuwa sehemu ya kufanikisha njama za kudanganya kwenye mitihani ili watahiniwa wafaulu kwa sababu wanafahamu athari zake.

Uandishi wa matusi badala ya majibu sahihi unaofanywa na baadhi ya watahiniwa wawapo kwenye vyumba vya mitihani, ni matokeo ya maadili mabaya waliyonayo baadhi ya wanafunzi.

Kwa mwanafunzi mwenye tabia njema, hawawezi kuandika matusi kwani ni mwenendo usiokubalika katika jamii. Naye ni tunda la jamii, ambalo limeendekeza matusi pendekezo.

Ni muhimu kwa wazazi na walezi kuwajenga watoto wao maadili bora ili waepukane na tabia mbaya ikiwemo kuongea matusi, kutukana, kufanya ishara za matusi na sasa kuyaandika kwenye mitihani ya kitaifa.

> Uandishi wa matusi badala ya majibu sahihi unaofanywa na baadhi ya watahiniwa wawapo kwenye vyumba vya mitihani, ni matokeo ya maadili mabaya waliyonayo baadhi ya wanafunzi.

Walimu kwa upande wao, wanayo fursa ya kuzuia uandishi wa matusi kwa kuwakumbusha mara kwa mara wanafunzi kuepukana na tabia hiyo mbaya. Wawakumbushe umuhimu wa kuzingatia maelekezo kwenye mitihani badala ya kufanya vitu visivyokubalika, kimsingi, mwanafunzi aliyejiandaa vyema kwenye mitihani hawezi kuandika matusi kwani malengo yake ni kufaulu ili avuke ngazi nyingine na kuwa mwenye mafanikio.

Ni muhimu wanafunzi kukumbushwa kuwa hata kama wamekosa majibu ya kujaza kwenye karatasi waepuke kuandika matusi kwa sababu ni afadhali kufeli mtihani kuliko kufutiwa matokeo kwa kuandika mambo ambayo ni fedheha kwao na shule pia.

Kama nchi, kuanzia ngazi ya familia hadi taifani lipo jukumu kubwa la ujenzi wa maadili mema katika jamii, kwa vile kukiwa na jamii yenye maadili mema, udanganyifu na matusi kwenye mitihani pamoja na tabia nyingine nyingi mbaya zitatoweka.

***Mwandishi ni mwalimu wa Mlali Sekondari iliyoko Kongwa mkoani Dodoma.***
***Mawasiliano : 620 800 462***

SAYANSI
NA MWANDISHI
WETU

# Usahaulifu, unene kupindukia magonjwa pasua kichwa yanayoelekea kukomeshwa

ZIPO fikra au hisia ndani ya jamii kuwa kunenepa kupindukia huonyesha uwezo wa fedha kwa imani kuwa kitambi ni heshima. Ni baada ya kuamini kuwa wanene wanakula vizuri na wembamba ni matokeo ya kukosa chakula.

Kiasi miaka inavyokwenda na ufahamu unavyoongezeka mambo hayo yanaelekea kufikia ukomo, kwa kuwa unene si afya wala jambo lenye tija au afya.

Kuwa bonge, pia watoto kuwa wanene kama wacheza sumo siyo tija wala heshima tena. Halafu si alama ya utajiri bali hatari kiafya.

Kuamini kuwa kunenepa ni jambo la maana na la muhimu ni uzamani hautakiwa kuwa na nafasi tena.

Imani hiyo inawalazimisha baadhi ya makabila kujitahidi kuwalisha wazazi na watoto wachanga ili wanenepe kama malkia wa nyuki ili inapotimia miezi mitatu baada ya kujifungua wawe na kilo 100.

Ikumbukwe kuwa kunenepa kupita kiasi ni tatizo linaliathiri mtu binafsi na pia kuongeza gharama kwa nchi, kuanzia matibabu kwenye sekta ya afya, inayogharamia tiba za figo, moyo na mishipa ya fahamu. Unene mkubwa hukwamisha uchumi na kutishia hatima ya nguvukazi.

Kwa mfano Marekani, karibu asilimia 70 ya watu wazima huathiriwa na uzito mkubwa na katika Ulaya idadi hiyo ni zaidi ya nusu.

Kunenepeana kupindukia kunahusishwa na kusababisha magonjwa kuanzia kisukari cha aina ya 2 (kinachoibuka ukubwani), maradhi ya moyo, mifupa (arthitis), ini na saratani fulani.



Unene kupindukia ni janga linalotikisa karibu dunia nzima. **PICHA: MTANDAO**

Mwaka jana umeshuhudia juhudi nyingi zikifanyika kukabiliana na janga hilo na aina mpya ya matibabu zinazidi kuibuliwa zikiondoa na kuleta matumaini kwamba upo uwezekano wa kumaliza tatizo hilo kwa kutumia 'glucagon- peptide-1 (GLP-1).

Hapo awali dawa hizo zilitengenezwa kwa ajili ya ugonjwa wa kisukari na sasa imegundulika kuwa vipokezi (receptors) vya GLP-1 mwilini husababisha kupunguza uzito kwa kiasi kikubwa.

Vita vya unene kupindukia vinaelekea kushinda kwa kuwapo na uhakika kwamba athari za dawa hizo zinazoweza kudhibitiwa.

Mwaka huo, majaribio ya kimatibabu yaligundua pia kuwa yalipunguza dalili za magonjwa ya moyo mfano kushindwa kufanyakazi na hatari ya mshtuko wa moyo na kiharusi kwa kutumia dawa hizo.

Ushahidi wa uwezo wa kumwezesha mtu kupata afya na faida kubwa zaidi ya kupunguza uzito kunawafanya wanasayansi kuitaja dawa za GLP-1 kuwa ni mafanikio ya mwaka 2023.

### KUMALIZA KUSAHAU

Zama hizi kusahau ni shida inayoelekea kumuumiza karibu kila mmoja. Ni , tatizo linalosumbua familia dunia nzima bila kujali ni za maskini au tajiri. Kusahau kunawaweka watu katika wakati mgumu kwa mfano mtu anaweza kuacha tena kushindwa kula.

Mwenye tatizo anaweza kukosa hamu ya kula , aidha kukataa vyakula au akawa anatema muda wote badala ya kumeza. Zipo nyakati anaweza kuwa na hasira hata kuwa na mwenendo wa tabia za kukikataa na kukikasirikia chakula jambo linalotishia hatima ya maisha yake.

Dawa za kutibu usahaulifu zimekuwa na mafanikio kiasi kidogo kuwaponya mamilioni duniani kote wenye ugonjwa wa Alzheimer (husomwa Alzeima), au usahaulifu.

Januari mwaka huu wasimamizi wa dawa Marekani wameiwashia nyota ya kijani dawa ya kwanza ambayo kwa mara ya kwanza kwa kiasi, inapunguza usahaulifu ikitambua na kuikabili kibaiolojia misingi ya ugonjwa huo.

Inatoa tumaini jipya kwa wagonjwa na familia zenye matatizo hayo japo bado kuna wasiwasi na hofu kuhusu tiba mpya kwa kuwa ni masuala yanayogusa ubongo, lakini angalau kuna mwanga.

Kitaalamu ubongo wa walio na ugonjwa wa Alzeima unakuwa na protini zinazoitwa 'beta amyloid', na kwa miaka mingi wanasayansi wanalumbana ikiwa kuziondoa kungesaidia wagonjwa. Tiba mbalimbali zilizofanya hivyo zilishindikana kurudisha akili.

Taarifa za karibuni zinasema matibabu mapya ya 'antiamyloid monoclonal' yanayoitwa 'lecanemab', yanapunguza au kudhibiti upotevu wa akili na utambuzi kwa asilimia 27, ikilinganishwa na tiba ya 'placebo,' ,

Hayo yanaibuka katika jaribio la msingi la miezi 18 , watalaamu wanasema ilitosha kuwashawishi wasimamizi wa dawa wa Marekani na baadaye Japan kuidhinisha tiba hiyo.

Katika matokeo ya majaribio matibabu mengine ya kingamwili (antibodies) ambayo pia yanalenga amyloid, yaitwayo 'donanemab'yalipunguza kupungua au kuharibika uwezo wa utambuzi kwa hadi asilimia 35 dhidi ya 'placebo' katika idadi ya wagonjwa tofauti kidogo, na idhini ya Marekani inaweza kuja siku yoyote kuruhusu tiba hiyo.

Dawa zote mbili zinatolewa kwa njia ya drip kwenye mishipa ya mgonjwa.

Ingawa watafiti wa Alzeima, madaktari, na wagonjwa wanasherehekea kupatikana dawa, wanaangalia upande wa pili kwenye hatari ya kutokea uvimbe ubongoni na kuvuja damu kwenye ubongo kunakotokana na matibabu, ambayo katika hali nadra limekuwa tatizo baya.Hata hivyo wanaamini kuwa kwenye nia kuna mafanikio.

**MITANDAO**

## Wajawazito wanapotumia dawa kwa njia hizi, wanajiangamiza na watoto wao

**INATOKA UK.11**

### MAONI WAFAMASIA

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafamasia Tanzania, Benson Katundu, anasema matumizi holela ya dawa kwa wajawazito ni tatizo, na hupewa dawa hizo kutoka kwenye maduka ya dawa kinyume na taratibu kwa sababu dawa za antibayotiki ni lazima ziandikwe na daktari ndipo zimfikie mgonjwa.

Anasema kwenye maduka ya dawa hakuna wataalamu wabobevu lakini baadhi yao siyo waaminifu na hata wengine kuweka dukani watu ambao hawana ujuzi wa dawa kutoa huduma hiyo na mgonjwa au mjazito akifika kuomba dawa fulani anapewa bila hata ya kuonyesha cheti cha daktari.

Anawataka wanaouza dawa kuishi taaluma yao na siyo kutanguliza pesa bali kujali afya za wananchi, wasiuze dawa bila cheti cha daktari au kuuliza tatizo la mgonjwa sababu ni wataalamu wafuate sheria, miongozo na maelekezo ya serikali kwenye kuhudumia wananchi."

Mmoja wa wauza dawa hapa mjini Shinyanga jina tunalo, anasema katika kuuza dawa hizo wote wanaokuja kununua ni wagonjwa husika, wengine hutuma watu kaninunulie dawa fulani, kumbe dawa hiyo anakwenda kupewa mjamzito na hatimaye kumletea madhara.

Anasema katika maduka mengi ya dawa ni mara chache kumuona mjamzito amekwenda kununua dawa, wengi hutuma watu wao wa karibu na kuelekezwa akanunue dawa fulani kwa mazoea bila ya kupata vipimo na kutokana na maduka ya dawa kuwa mengi muuzaji hawezi kuuliza uliza maswali itabidi auze dawa na kuingiza pesa.

### MPANGO KITAIFA

Mipango ya serikali kudhibiti matumizi holela ya dawa, inaainishwa kwenye tovuti ya Wizara ya Afya, Waziri wa Afya Ummy Mwalimu anasema, serikali imeweka mikakati ya kukabiliana na tatizo la matumizi holela ya dawa hasa antibayotiki.

Mikakati hiyo ni pamoja na kuondoa usimamizi wa maduka ya dawa kutoka Baraza la Famasi na kupeleka kwenye Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba TMDA.

Aidha, tatizo hilo la matumizi holela ya dawa, linachochewa na baadhi ya wataalamu ambao wanakwenda kinyume na kanuni na miongozi ya taaluma yao, na Waziri anawataka wahudumu wa afya, madaktari na wafamasia kusimama kwenye taaluma zao na kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya dawa.



## Serukamba awafunda maofisa biashara

**Na Mwandishi Wetu,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewataka maofisa biashara nchini kutoa elimu kwa wananchi ya umuhimu wa urasimishaji wa biashara ili kuwapunguzia gharama zisizo halali.

Serukamba alitoa wito huo jana wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa hao wa mikoa ya Dodoma, Singida, Rukwa, Simiyu, Katavi na Tanga yanayofanyika mji hapa.

Alisema serikali imekuwa ikipinga gharama zisizo halali za urasimishaji biashara vitendo vinavyofanywa na watu wasio waadilifu.

"Mafunzo haya ni muhimu kwa kuzingatia kuwa hivi sasa masuala ya uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji ikiwemo utoaji wa huduma za Leseni za Biashara na Viwanda yanafanyika kwa njia ya mtandao kupitia Mifumo ya Kielektroniki au mifumo ya TEHAMA," alisema Serukamba

Alisema ni matumaini yake kuwa mafunzo hayo yatakuwa chachu kwa maofisa hao kuboresha utoaji wa huduma kwa wafanyabiashara na wawekezaji.

Alisema mafunzo hayo ni nyenzo ya kupunguza kero na gharama za urasimishaji biashara, ikiwa ni utekelezaji wa uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini.

Serukamba aliongeza kuwa mafunzo hayo yamezingatia umuhimu wa maofisa hao kuwa karibu na wananchi kwa kutoa huduma bora ili kukuza kipato, Serikali kupata kodi na uchumi wa nchi kuimarika.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Godfrey Nyaisa, alisema maofisa hao wanatakiwa kuachana na mtazamo wa kuwa wakusanya mapato pekee na kufunga biashara za watu.

Aliwataka kuwatambua wafanyabiashara katika maeneo yao, kusikiliza kero zinazosababisha kufunga biashara na kuzitafutia majawabu ili biashara zao ziendelee kuimarika.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na BRELA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Viwanda na Biashara yana lengo la kuwajengea uwezo maofisa biashara nchini.

# Mkalama wajihami kwa kipindupindu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

WILAYA ya Mkalama mkoani Singida imeanza kujihami kwa kipindupindu kwa kuwaagiza maofisa tarafa, watendaji kata na vijiji kuwakamata na kuwatoza faini wananchi wasiokuwa na vyoo ili kudhibiti mlipuko wa ugonjwa huo.

Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali, alitoa agizo hilo juzi kwenye mkutano na wakuu wa idara, watendaji hao, maofisa tarafa hao na watumishi wa afya wa kujadili namna ya kukabiliana na ugonjwa huo.

Machali alisema viongozi hao wanapaswa kuhakikisha kila kaya inakuwa na choo, lasivyo watozwe faini.

"Sitaki kusikia mtu hana choo na pia natoa miezi mitatu kwa shule zote ziwe na vyoo na ambazo hazina wananchi wachangishwe michango ya ujenzi."

"Waelimisheni mamalishe, babalishe, wachoma mahindi wazingatie usafi, wananchi watumie maji ya kuchemsha au yaliyotibiwa kwa dawa na vilabu vyote vya pombe ambavyo havina vyoo vifungwe mara moja," alisema.

Alisema serikali inataka kuona kila kaya inakuwa na choo ili kupambana na tishio la mlipuko wa kipindupindu wilayani Mkalama.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Asia Messos, aliwataka walimu kuhakikisha wanawaelimisha wanafunzi dhidi ya kipindupindu kwa kuzingatia matumizi ya majisafi na salama na kuweka vyoo vya shule safi muda wote.

Messos aliwataka watendaji hao ambao maeneo yao yanatekeleza miradi mbalimbali kusimamia vizuri na kuweka bajeti nzuri ili kuepukana kutokamilika kwa wakati.

"Kila mwenye mradi asimamie mradi wake mpaka ukamilike, tuzingatie bajeti, umepokea pesa kaa chini fanya tathimini kulingana na bajeti uliyopewa hii itatusaidia tuondokane na tatizo la miradi kutokukamilika na ukiona mradi unachangamoto yeyote tuambiane," alisema.

Akiwasilisha taarifa ya orodha ya vijiji vitakavyonufaika na fedha za jimbo kwa mwaka wa fedha 2023/24, Ofisa Mipango Wilaya hiyo, James Paul alisema serikali imetoa Shilingi milioni 72.9 kukamilisha miradi ya afya na elimu.



Kiongozi wa Timu ya Kampeni ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Malongo Jackson, akitoa elimu kwa wananchi wa Kijiji cha Ipande mwishoni mwa wiki walipofika kutoa maoni yao kupitia kampeni hiyo inayoendelea mkoani Singida. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RITA yashauri jamii kuandika wosia

**Na Ibrahim Joseph,**
SINGIDA

WAKALA wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) umeishauri jamii kuandika wosia ili kuepuka migogoro ya mgawanyo wa mali.

Ofisa wa RITA, Mohamed Changula alitoa ushauri huo kwenye mkutano wa hadhara wa Kijiji cha Ipande Halmashauri ya Wilaya ya Itigi mkoani humo mwisho mwa wiki iliyopita wakati wa kutoa elimu ya msaada wa kisheria kupitia Kampeni ya Mama Samia.

"Kuandika wosia sio kujichuria kifo kama jamii inavyoamini bali ni utaratibu wa kuandaa mgawanyo wa mali zako ili kuondoa mgogoro pale kifo kitakapokuchukua," alisema.

Alisema kuna aina mbili za kuandika wosia, kwa njia ya maandishi na mdomo na kunatakiwa kuwepo mashahidi na kubaki kuwa siri ili kuepusha mgogoro kwa warithi walioandikiwa.

Alisema wosia huo baada ya kuandikwa ni lazima uthibitishwe na mwanasheria na mhusika anaweza kuomba uhifadhiwe ofisi za RITA kwa usalama.

Changula alisema wosia unaanza kufanya kazi pale mhusika anapofariki na mashahidi watawasiliana na ofisi kuwajulisha ili kufikishwa kwenye kikao cha familia.

Alisema wanaojitoa kwenye wosia ni watakaofanya jaribio la kutaka kumuua mzazi na wale ambao hawatamhudumia mzazi alipokuwa mgonjwa.

Kuhusu taratibu za usimamizi wa mirathi , alisema wanafamilia wanatakiwa kukaa kikao cha watu wasiopungua wanane kati ya hao, wanne wawe na kitambulisho cha taifa.

Kiongozi wa kampeni hiyo wa wilaya hiyo, Malongo Jackson, alisema lengo la ni kutoa elimu ya msaada wa kisheria na kutatua kero za wananchi.

Jackson alisema kampeni hiyo kimkoa ilizinduliwa Januari 10, mwaka huu na kugawanyika kila wilaya kusikiliza kero za wananchi kupitia mikutano ya hadhara na mtu mmoja mmoja.

Alisema kero nyingi walizokutana nazo ni migogoro ya ardhi, ndoa na unyanyasaji wa kijinsia.

Kwa mujibu wa Jackson, kampeni hiyo ina wataalamu wa kisheria kutoka ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii na na madawati ya kijinsia wa Jeshi la Polisi.





# Serikali yaingiza Tril. 2.9/- mazao ya mkakati nje

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

VYAMA vya ushirika vimeingizia serikali zaidi ya Shilingi trilioni 2.9 kwa kuuza mazao ya kimkakati yanayozalishwa nchini kwa kipindi cha miaka miwili ya fedha.

Takwimu hizo zimetolewa na Naibu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini Divisheni ya Usimamizi na Udhibiti, Cillin Nyakunga, wakati anafungua mafunzo maalum kwa maofisa ushirika wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yanayofanyika kwa wiki mbili jijini Mbeya.

Aliyataja baadhi ya mazao hayo kuwa ni korosho, tumbaku, soya, dengu, kahawa, chai, pamba, choroko na mkonge ambayo yanazalishwa katika mikoa mbalimbali nchini.

"Mazao haya yote yaliuzwa kupitia vyama vya ushirika, lakini takwimu hizi ni za miaka miwili ya fedha ya mwaka 2021/2022 na 2022/2023 kwa hiyo haya ni mazao muhimu sana kwa uchumi wa taifa letu," alisema Nyakunga.

Mwakilishi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angela Maganga alisema tatizo linalowakumba maofisa ushirika walioko kwenye halmashauri ni sheria kutoweka wazi baadhi ya majukumu yao.

Angela alisema taratibu zinawataka kuhamasisha vyama vya ushirika kuanzishwa, lakini hawajapewa mamlaka ya wazi kusimamia vyama hivyo hali ambayo wakati mwingine husababisha mikanganyiko ya uendeshaji wake.

Alisema sheria hazijawapa mamlaka ya kusimamia vyama hivyo baada ya kuhamasisha vianzishwe na kwamba tatizo hilo limekuwa likiathiri utendaji kazi wao.

Baadhi ya maofisa ushirika wanaoshiriki mafunzo hayo, waliahidi kuongeza weledi wa uendeshaji wa vyama hivyo kwenye maeneo yao na kuongeza ufanisi.

Mmoja wa maofisa hao, Zwai John ambaye ni Ofisa Ushirika kutoka mkoani Katavi aliishukuru Serikali kwa kuwapatia mafunzo hayo kwani yatawasaidia kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Alisema mafunzo hayo yatawasaidia kujifunza na mbinu ambazo walikuwa hawana za uendeshaji wa vyama hivyo kwenye maeneo yao.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Mohamed Fakii aliwataka maofisa ushirika hao kutatua migogoro ambayo inaibuka kwenye vyama hivyo kwa kuwa ndiyo inavuruga uendeshaji wake.

Alisema baadhi ya migogoro hiyo imekuwa ikiibuka baina ya wanachama, mingine ni ya chama kimoja na kingine na kupunguza ufanisi.



Baadhi ya wachuuzi wa mboga pembeni mwa kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho Dar es Salaam, wakiwa wameshuka kutoka eneo la juu (kulia) na kupanga biashara zao chini juzi, kitendo ambacho husababisha usumbufu kwa wapitanjia. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mwekezaji alia na polisi

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

JESHI la Polisi mkoani hapa limelalamikiwa kwa kushindwa kurejeshwa kwa bidhaa zilizoibiwa katika Kiwanda cha Kuzalisha Mifuko ya Plastiki kilichoko katika mji wa Mbalizi mkoani hapa kwa zaidi ya miezi saba licha ya wahusika kukamatwa.

Malalamiko hayo yalitolewa na wawekezaji wa kiwanda hicho wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ya kutembelea viwanda mbalimbali mkoani hapa kwa lengo la kusikiliza kero zao na kukagua mwenendo wa uendeshaji.

Meneja uzalishaji wa kiwanda hicho, Lameck Elias alisema Julai mwaka jana kuna watu walivamia kiwandani hapo na kuiba mabelo 70 ya mifuko na na kuwasababishia hasara.

Alisema walitoa taarifa polisi kuomba msaada wa kuwasaka watuhumiwa na kufanikiwa kuwakamata na kutakiwa kurejesha mifuko hiyo.

Alisema watuhumiwa walirejesha mabelo hayo ambayo hayafiki hata nusu ya yale yaliyokuwa yameibwa na yaliyobaki imekuwa kizungumkuti na kuzua wasiwasi kwa kiwanda hicho.

"Polisi walituahidi wanalishughulikia lakini mpaka sasa wako kimya, sasa tunashindwa kuelewa kwa nini maana wahusika walikamatwa na wakarejesha mabelo mengine," alisema Lameck.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliliagiza jeshi hilo kushughulikia tatizo hilo haraka kwa kuhakikisha watuhumiwa hao wanarejesha mifuko yote waliyoiba ili wawekezaji hao waendelee kufanya kazi kwa amani.

Homera alisema kama watuhumiwa walikamatwa hakuna sababu kwa jeshi hilo kushindwa kuwalazimika kurejesha bidhaa hizo.

"Kama wahusika walikamatwa na wakarejesha karibia nusu ya mabelo hayo, inashindikanaje maabelo yaliyobakia kutorejeshwa," alihoji Homera.

Aliliagiza jeshi hilo kushughulikia kero hiyo ndani ya wiki moja ili wawekezaji hao waendelee na shughuli zao za uzalishaji bila kikwazo.

Akimwakilisha Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ofisa Polisi Jamii wa Mkoa huo, George Salala alisema tatizo la wizi kwenye viwanda kikiwemo hicho lipo.

Alisema wamekuwa wakishirikiana na wawekezaji kuhakikisha matukio ya aina hiyo hayatokei na kwamba tukio la wizi uliotokea kwenye kiwanda hicho aliwahi kulisikia na kuahidi kufuatilia ili mwisho wake ujulikane.

Alisema baada ya kulifuatilia watatoa taarifa ndani ya muda mfupi kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huku akisisitiza kuwa watahakikisha maeneo yote ya wawekezaji yanakuwa salama.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya pia ilitembelea Kiwanda cha Saruji cha Songwe na viwanda vya vinywaji vikali na baridi vilivyopo Iyunga jijini Mbeya.

## Wakulima wa parachichi wakabidhiwa vyeti

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA 300 wa parachichi wamepatiwa vyeti vya ithibati kwa kukidhi viwango vya kimataifa katika Soko la Ulaya.

Vyeti hivyo vimetolewa na asasi ya kilele inayojishughulisha na kilimo cha mboga, matunda na mimea itokanayo na mizizi na viungo ya Tanzania Horticultural Association (TAHA).

Hayo yalisemwa na Mratibu wa Maendeleo Biashara kutoka TAHA, Asia Barnabas, baada ya mkutano wa Jukwaa la Wadau wa Parachichi uliofanyika mkoani hapa.

Asia alisema malengo ni kuhakikisha parachichi inayolimwa Tanzania inafikia masoko makubwa duniani.

"Na ili parachichi iweze kufikia masoko inatakiwa ianze kuwa na ubora kuanzia inapozalishwa, lakini tunaiomba sasa serikali yetu ya mkoa na serikali kuu kuhakikisha hizi changamoto ya kimiundombinu zinazosababisha parachichi hii pendwa isimfikie mlaji au isifikie soko ziangaliwe," alisema.

Hata hivyo, Asia alisema hakuna namna ya kufikia Soko la Dunia bila ya kuhakikisha kwamba changamoto kwa wakulima na wafanyabiashara zinatatuliwa.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka aliwaagiza Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuhakikisha kila taasisi inatatua changamoto katika eneo lake.

"Muanze mara moja mpango wa kujenga barabara zinazoelekea maeneo ya uwekezaji mkubwa, pia mnatakiwa kusogeza huduma ya umeme ili utumike kwa umwagiliaji mashambani na uchimbaji wa visima virefu kwa mkulima mmoja mmoja," alisema.

Alisema kabla ya kufikia hatua za kuchukua ushuru kwa wakulima ni vyema huduma hizo zikaboreshwa ili wakulima waweze kuzalisha mazao kwa tija na ubora unaotakiwa katika soko la dunia.

Mmoja wa wakulima hao, Edger Mtitu alisema endapo mkakati wa kilimo na masoko uliowekwa na serikali utafuatwa utaleta mageuzi katika uzalishaji pamoja na uchumi.

Aliomba serikali kudhibiti makampuni ambayo yananunua mazao ikiwemo parachichi katika Mkoa wa Njombe na kuyagonga nembo za mataifa mengine kwa sababu wanaondoa uhalisia wa zao husika.





# Kadogosa azungumzia usafirishaji mizigo Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Shirika la Reli Tanzania (TRL), Masanja Kadogosa amesema mpango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kurejesha usafiri wa reli utapunguza gharama za usafirishaji wa mizigo visiwani hapa.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa TRL, Masanja Kadogosa katika maonyesho ya biashara yanayoendelea katika viwanja vya Nyamanzi ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi ambayo kilele chake kilifanyika wiki iliyopita.

Kadogosa alisema reli hiyo ilidumu kwa miaka 25 na kufungwa mwaka 1930, hivyo kuwepo kwa TRL visiwani Zanzibar ni jambo jema hasa ikizingatiwa kuwa SMZ inatarajia kurejesha reli.

Alisema historia ya reli ilianza visiwani hapa mwaka 1879 baada ya reli ya kwanza kujengwa na utawala wa Kisultani kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema TRL litakuwa washiriki wazuri kwa sababu wana wahandisi wa kutosha na uzoefu wa kujenga reli, kutoa ushauri wakati Zanzibar inatarajia kujenga reli.

Alisema usafiri wa reli ndio pekee wenye gharama nafuu hasa katika usafirishaji wa mizigo. Alisema shirika hilo litakapomaliza ujenzi wa reli gharama za usafirishaji wa bidhaa zitashuka na mfumuko wa bei za bidhaa kupungua.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa reli ya SGR, alisema unaendelea vizuri licha ya kukabiliwa na changamoto ambazo zinaendelea kufanyiwa kazi.

Aliwapongeza viongozi wa kitaifa kwa uamuzi wa ujenzi huo kuwa utasaidia kuleta maendeleo nchini.

"Ujenzi huu ni mkubwa na umegharimu fedha nyingi, mpaka sasa Sh. bilioni 10.3 zimeshatumika katika ujenzi huu, tuwashukuru sana viongozi wetu na ujenzi huu utakapomaliza hata bei ya mchele Zanzibar itashuka," alisema.

Alisema ujenzi huo unatarajiwa kukamilika Julai 30 mwaka huu na kusafiri kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (wa pili kushoto), akimkabidhi Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Juma Kimori (wa pili kulia), cheti cha shukrani ya udhamini wa Kombe la Mapinduzi wakati wa fainali ya mashindano hayo mwishoni mwa wiki. Benki hiyo ilidhamini michuano hiyo kwa Sh. milioni 200. Kushoto ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla na kulia ni Meneja wa Biashara Zanzibar wa Benki ya NMB, Naima Said Shaame. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Wananchi waelimishwe biashara'

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe ameziтaka taasisi za biashara kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kujenga uelewa wa majukumu yao na biashara nchini.

Kigahe alisema Tanzania inategemea biashara hivyo ni vyema kutoa elimu ya umuhimu wake na kuondoa malalamiko ya wafanyabiashara na wananchi.

Aliyasema hayo katika ukumbi wa Dk Mwinyi uliopo Nyamanzi Wilaya Magharib B' Unguja wakati akifungua mkutano wa wakuu wa taasisi za serikali nchini.

Alisema wafanyabiashara wengi hawana uelewa juu ya makato na tozo za biashara kati ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kuzua malalamiko hivyo kuna haja kwa taasisi hizo kuendelea kutoa elimu ya kuwajengea.

Alisema kuna changamoto nyingi katika taasisi za biashara, hivyo ni vyema kushirikiana kutoa fursa kwa wafanyabiashara kuendelea na biashara zao na kuleta maendeleo.

"Sisi tuna haja ya kusimamia na kutekekeza malengo ya biashara ili kuleta mafanikio yetu katika Muungano wetu," alisema Naibu waziri huyo.

Alisema Tanzania Bara na Zanzibar ni nchi moja, hivyo ni vyema kushirikiana ili kuleta mafanikio.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban alisema wizara hiyo ipo tayari kutoa ushirikiano kwa wafanyabiashara ili kukuza pato la taifa.

Shaaban aliwataka watendaji wa serikali kuzingatia mipango madhubuti waliyojiwekea ili kufikia malengo waliyokusudiwa.

Akiwasilisha maazimio ya mkutano huo, Mwenyekiti wa Jukwaa la Taasisi hizo, Latifa Khamis, alisema jukwaa la viongozi wa mashirika na taasisi za umma kutoka SMZ wamedhamiria kukamilisha usajili ifikapo robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema jukwaa hilo limedhamiria kutoa ushirikiano wa kiutendaji kwa jukwaa tarajiwa la watendaji wakuu la SMZ katika kurasimisha jukwaa hilo kupitia usajili rasmi.

Aliwataka wakurugenzi wakuu kufanya kazi kwa bidii ili kutimiza malengo ya taasisi na dhamira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia na Rais wa SMZ, Dk. Mwinyi kuchochea utoaji huduma bora katika taasisi hizo.

## Korea yapongezwa kwa misaada Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo , Mifugo, Umwagiliaji na Maliasili Zanzibar, Shamata Shaame Khamis ameipongeza Serikali ya Korea Kusini kwa kuipatia Serikali ya Zanzibar misaada.

Khamis alisema misaada hiyo inayotolewa kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada la China (KOICA), ikiwemo elimu ni muhimu na ndio maana Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Aman Karume alitangaza itolewe bure.

Akizungumza katika Shule ya Sekondari Chwaka Tumbe wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la bweni la wasichana linalojengwa na Taasisi ya KFHI kwa ufadhili wa KOICA, alisema Mapinduzi ya mwaka 1964 yameleta uhuru, umoja na mshikamano , hivyo ni vema kuyalinda na kuyatetea.

Aliitaka serikali kuona umuhimu wa kuboresha mazingira ya elimu ikiwemo ujenzi wa majengo ya kisasa na kuongeza maslahi walimu ili kufanya kazi zao kwa weledi.

Alisema kutokana na mazingira hayo ya kujisomea kuwa mazuri kumekuwa na ongezeko la ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya taifa.

Mtedaji Mkuu wa KFHI, Sommie Koh alisema kukamilika kwa bweni hilo kutawapa fursa wasichana kupata fursa ya kupitia masomo yao kwa utulivu.

Mkurugenzi wa KOICA Tanzania, Jongbun Joo alisema Tanzania ni moja ya nchi kubwa ambayo wanashirikiana nayo kufanikisha miradi mbalimbali ikiwemo ya elimu.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk aliwataka wazazi kuacha kuwapa majukumu makubwa watoto wa kike na kuacha kuwaozesha mapema kabla ya kumaliza masomo yao na kuwahimiza kusoa kwa bidii ili watimize ndoto na taifa kupata wataalamu .

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mwanakhamis Adam Ameir alisema bweni hilo lina uwezo wa kuchukua wanafunzi wa kike 80 kwa wakati.

**Aliitaka serikali kuona umuhimu wa kuboresha mazingira ya elimu ikiwemo ujenzi wa majengo ya kisasa na kuongeza maslahi walimu ili kufanya kazi zao kwa weledi.**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA



Ndugu **ABBAS IDD RAMADHANI** (pichani) anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE485675** iliyotolewa na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Jun 2022. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba ***PHQ/KAG/BUK/273/2024.*** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAADA SAADALLAH** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba P0320/0508 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIGOMA SEKONDARI CENTRE** mwaka 2006. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: PHQ/KIG/KIG/89/2024.

## KUPOTEA KWA CHETI



**JANE MARCO MKUMBO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No.S 2644/0035 kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa kupitia KINAMPANDA SECONDARY SCHOOL mwaka 2019 namba ya cheti Cs19164396. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/967/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACQUELINE SORAEL PALANGYO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S/0557/0029** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NARUMU SECONDARY SCHOOL** mwaka 2005. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/798/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA KILOMBERO**
**KITUO CHA MKAMBA, MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA NDOA NA. 1/2024**
**JINA LA MDAI: EMELICK FRANCIS LIHEKA**
**DHIDI YA**
**JINA LA MDAIWA: SALEJA ANGOLILE**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**KWA: SALEJA ANGOLILE**
**Kwakuwa mdai/wadai ameleta /wameleta madai yake/yao kwamba:**
**UNAHITAJIKA UFIKE HAPA MAHAKAMANI KUJIBU SHAURI LA TARAKA.**

Hivyo Unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakamana hii siku ya Alhamisi tarehe 18 Mwezi 1 Mwaka 2024 saa3:00 Asubuhi na kwa mujibu wa madai hayo na kwakuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hukudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitisha kuwa umepokea Hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 8 mwezi 1 Mwaka2024.

..............................
**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO MKAMBA**
**WILAYA YA KILOMBERO**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya NACHINGWEA**
**Kituo cha KILIMARONDOMkoa LINDI**
**Shauri la Madai Na. 8/2024**
**Jina la mdai SUWEDI AMANI KUCHUPA**
**Jina la mdaiwa DIMIKI MLEMELA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa DOMINIKI MLEMELA**
**MKAZI WA NAGAGA MAJENGO MATEKWE**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba ( Eleza hapa habari za madai)**
**YA FEDHA KIASI CHA TSH 950000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 25 Mwezi 1 Mwaka 2024 saa 2;00 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 4 mwezi 1 mwaka 2024

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA WILAYA SONGWE**
**LILILOPO MBOZI**
**SHAURI NA. 82/2023**
**1.BRAYAN SICHIVULA::::::::::::::::::MDAI**
**2.PEPE GREEN SICHIVULA:::::::::::::MDAI**
**3.MAPALALA MAGAMBO:::::::::::::MDAI**
**4.RAISI JOEL KIBONA::::::::::::::::::::MDAI**
**5.ASUMILE BENSON SHIMWELA:::MDAI**
**DHIDI YA**
**1.SHABAN MWASOPO:::::::::::::::MDAIWA**
**2.GREEN SICHIVULA::::::::::::::::::MDAIWA**

**YAH : KUITWA SHAURINI**
**KWA: SHABANI MWASOPO**

Fahamu kwamba **BRAYAN SICHIVULA** na wenzake wa Nne,wamefungua shauri dhidi yako katika Baraza hili.
Shauri limepangwa kusikilizwa tarehe 19/01/2024 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere,Mwenyekiti wa Baraza.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosqa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Mnadani Vwawa.
**Kumbuka:** Usipo hudhuria siku hiyo hukumu itasomwa pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 07/12/2023.

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**07/12/2023**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**SAIDI MOHAMEDI NYANGE** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki. **MC 259 AQZ** aina ya **SKYMARK. MC 408 BSC** aina ya **HUONIAO. MC 178 CQM** aina ya **KINGLION.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/TAN/TAN/399/2024.**

## HATI YA KIAPO CHA KUBADILI MAJINA



Mimi **RAHMA ATHUMANI SENGO** umri miaka 60, kabila Mmakonde, Mkazi wa Magomeni, Mkoa wa Dar es salaam, Dini Muislam, nikiwa na akili zangu timamu na bila kushawishiwa na mtu yeyote naapa na kuthibitisha mbele ya Mahakama hii kama kwamba:-

1. Mimi nimekuwa ninatumia majina mawili tofauti ambayo ni **RAHMA ATHUMANI SENGO** na **RAHMA ISMAIL JUMA.**
2. Kwamba, **ISMAIL JUMA** ni ubini wa mume wangu na **ATHUMANI SENGO** ndio ubini wa baba yangu mzazi.
3. Kwamba, baadhi ya nyaraka zangu zilizobeba majina hayo ni pamoja na kitambulisho changu cha Taifa, nyaraka zangu za PPF na Benki.
4. Kuanzia leo naacha rasmi kutumia jina moja kati ya hayo, yaani **RAHMA ISMAIL JUMA** ambayo hasa kadi yangu ya PPF na Benki. Badala yake nijulikane kwa jina la **RAHMA ATHUMANI SENGO.**
5. Kwamba, nimeamua kutumia jina hilo la **RAHMA ATHUMANI SENGO** kwa sababu ndilo jina lenye ubini sahihi wa baba yangu mzazi.

Nazidi kusisitiza kwamba kuanzia leo hii mahali popote nitambulike kwa jina **RAHMA ATHUMANI SENGO** badala ya **RAHMA ISMAIL JUMA** na endapo itagundulika vinginevyo hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu mtoa tamko hilo.
Kwa kuwa mtoa kiapo hiki ni mtu mzima na mwenye akili timamu nathibitisha kiapo chake leo hii.

**Imeshuhudiwa na;**

JINA ....ZULFA NGELANGELA....
CHEO ....HAKIMU....
SAHIHI ....................
TAREHE ....1/2/2023....

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB:**
**+255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,
KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Chama tawala DR Congo chaongoza wingi viti ubunge

**KINSHASA,** DRC

TUME ya Uchaguzi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), kwa mara nyingine imetangaza ushindi wa nafasi za ubunge kwa Chama cha UDPS kinachoongozwa na Rais Felix Tshisekedi.

Katika matokeo hayo yaliyotangazwa juzi Jumapili, chama hicho kimetwaa nafasi 66 za ubunge, kati ya 500 zilizopo, idadi ambayo hakuna chama kingine kilichoifikia, hivyo kukipa mamlaka ya kuamua kisheria bungeni chama hicho.

Vilevile, matokeo ya tume yanaonesha kuwa, vyama ambavyo walau vimekaribia idadi hiyo ni vya baadhi ya washirika wa Rais Tshisekedi, akiwamo Spika wa Seneti Modeste Lukwebo, Waziri wa Ulinzi Jean Bemba na Waziri wa Uchumi Vital Kamerhe vilivyoshinda zaidi ya viti 80 vya ubunge.

**Pia inatajwa kuna vyama vingine 44 vilivyopata wastani wa kiti kimoja au idadi inayokaribia na hiyo.**

Pia inatajwa kuna vyama vingine 44 vilivyopata wastani wa kiti kimoja au idadi inayokaribia na hiyo.

Matokeo ya kura ya ubunge yalitolewa baada ya Mahakama ya Katiba kuthibitisha kuchaguliwa Rais Tshisekedi katika uchaguzi unaodaiwa kuwa na kasoro nyingi, za kura kutopigwa kwa wakati na maeneo mengine kupigwa kwa siku ambayo haikupangwa.

Vyama vya upinzani na waangalizi huru wa uchaguzi walieleza wasiwasi wao kuhusu uwazi wa uchaguzi huo, wakitoa mfano wa machafuko, masharti ya upigaji kura na mchakato wa kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Hata hivyo, serikali kadhaa za nchi za magharibi zilimpongeza Rais Tshisekedi kwa kuchaguliwa na anatarajiwa kuapishwa ili kuongoza muhula mwingine wa miaka mitano kama kiongozi wa nchi ya pili kwa ukubwa barani Afrika baada ya muhula wa kwanza uliokumbwa na matatizo ya kiuchumi na mgogoro wa kiusalama kwenye mikoa ya mashariki.

Kupingwa kwa matokeo ya uchaguzi kunatishia kuiyumbisha zaidi DRC, nchi ya tatu kwa uzalishaji wa shaba duniani. Huku vyama vya upinzani vikilaumu mara kwa mara kwamba uchaguzi huo ulijaa mikasa ya udanganyifu, vikidai uchaguzi huo urudiwe, lakini hoja hiyo haikuridhiwa na mahakama.

Tume ya Uchaguzi (CENI) imejitetea kwamba uchaguzi ulikuwa wa kuaminika, ingawa ilibatilisha matokeo ya wagombea 82 wa nafasi za ubunge kati ya wagombea 100,000 kwenye uchaguzi wote uliofanyika Desemba mwaka jana. **DW**

## Kagame: Hakuna wa kutupangia cha kufanya

**KIGALI,** Rwanda

RAIS wa Rwanda, Paul Kagame amesema hakuna chombo chochote kutoka nje ya nchi hiyo ambacho kinaweza kuiamuru Rwanda njia ipi ipite na kuuamuru uongozi nini cha kufanya akieleza kuwa jukumu hilo ni la Wanyarwanda wenyewe.



Akizungumza jana wakati wa maombi ya kitaifa nchini humo, Kagame alisema watu wote wapo sawa mbele za Mungu na kwamba hakuna ambaye yupo juu kuliko mwingine, akisisitiza kuwa ukweli huo uwe chanzo cha kuwapa hamasa na msukumo utakaowapa mwongozo wa matendo yao kwenye masuala mbalimbali.

"Kwa kuzingatia historia ya Rwanda, changamoto tunazozipitia sasa na malengo yetu ya baadaye, ni dhahiri kwamba hakuna chombo chochote kutoka nje bila kujali asili yake ambacho kinaweza kutuamrisha njia ipi nchi yetu ipite, kutuamrisha uongozi wetu uweje na wapi tuelekee, jukumu hilo ni letu sisi Watu wa Rwanda wenyewe," alisema na kuongeza.

"Haijalishi unatokea wapi lakini kama una maoni mazuri ambayo yanatofautiana na yangu nitakusikiliza na tutafanya mazungumzo lakini siwezi kukubali amri ya mtu yoyote kutoka kwa wale wanaodhani ni bora kuliko sisi sote na wanaodhani wana haki kwenye huu utawala, siwezi kukubali," alisisitiza.



Raia wa Comoro wakipiga kura juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Upinzani Comoro walalamikia udanganyifu uchaguzi

**MORONI,** Comoro

VYAMA vya upinzani nchini Comoro vimelalamikia uchaguzi uliofanyika katika taifa hilo juzi kwamba ulijaa udanganyifu na kwamba unatarajiwa kutoa ushindi wa muhula wa nne wa miaka mitano kwa Rais Azari Assoumani.

Ilielezwa kuwa uchaguzi huo ulifanyika wakati wapinzani watano wakidai ulijawa na udanganyifu, na kwamba baadhi ya masanduku ya kupigia kura tayari yalikuwa yamejazwa kura za kumchagua Rais Assoumani anayeongoza taifa hilo.

"Kama ilivyokuwa mwaka 2019, tunashuhudia udanganyifu mwingine kwenye uchaguzi ukifanywa na Azali Assoumani akishirikiana na jeshi," alisema mmoja ya wagombea wa kiti cha Urais, Mouigni Soilihi.

Pia ilielezwa kuwa zoezi la upigaji kura lilianza kwenye visiwa hivyo vya bahari ya Hindi saa 2:00 usubuhi, likishirikisha wapiga kura 338,940 waliojiandikisha kati ya jumla ya wakazi 800,000.

Hata hivyo ilibainishwa kuwa upigaji kura ulimalizika saa 12 za jioni, na kwamba zoezi la kuhesabu kura linaendelea licha ya madai ya upinzani ya kuwepo kwa vitendo vya udanganyifu.

Baadhi ya viongozi wa upinzani walidai kuwa tume ya uchaguzi inapendelea chama tawala, suala ambalo tume hiyo imekanusha na kusema kwamba zoezi hilo litakuwa lenye uwazi.

Rais Assoumani anayechuana na wagombea wengine watano alisema anatumai kushinda katika duru hiyo ya kwanza ya uchaguzi.

"Kuna imani kwamba nitashinda kwenye duru hii ya kwanza, ni Mwenyezi Mungu ndiye atakayeamua na watu wa Comoro. Na ikiwa nitashinda kwenye duru ya kwanza, tutaokoa muda na fedha," alisema Rais Assoumani.

Rais Assoumani ambaye anadaiwa kuwakabili wakosoaji wake kwa mkono wa chuma ikiwamo kuwafunga jela na kuwalazimisha wengine kwenda uhamishoni alikanusha madai ya dosari kwenye uchaguzi huo.

Miongoni mwa dosari zilizotajwa ni hitilafu kwenye vituo vya kupigia kura ambazo alisema hajazisikia na kuhusu idadi ndogo ya wapigakura waliojitokeza, Rais Assoumani alisema hilo limechangiwa na hali mbaya ya hewa husasani mvua iliyokuwa inanyesha siku ya kupiga kura.

Ilibainishwa kuwa kwenye maeneo kama La Coulee, wilaya iliyo kusini mwa mji mkuu, kura zilikuwa zikihesabiwa kwa mwanga wa mshumaa huku ulinzi mkali wa polisi ukishuhudiwa nje ya vituo.

Msanii maarufu visiwani Comoro wa miondoko ya kufokafoka Cheikh MC, ambaye alikuwa mmoja ya waangalizi wa kuhesabu kura kwenye eneo hilo, alisema hakuvutiwa na zoezi lililokuwa linakwenda.

"Kwangu mimi, huu siyo uchaguzi. Tunashuhudia mchezo mchafu unaoweza kuleta balaa," alisema.

Naye, meneja wa kampeni za Rais Assoumani, Houmed Msaidie aliyapinga madai yote ya kuwepo wizi au udanganyifu, akiwatuhumu upinzani kupiga kelele kwa vitu vidogo na dhana zisizo na ukweli.

Rais Assoumani, ambaye anatawala visiwa vya Comoro tangu mwaka 2016 alirefusha muhula wake madarakani kupitia mabadiliko tata ya katiba.

Mabadiliko ya katiba ya baada ya uchaguzi wa rais wa mwaka 2019 yaliyoondoa sharti la nafasi ya urais kuwa ya kupokezana miongoni mwa visiwa vitatu vikubwa vinavyounda Jamhuri ya Comoro.

Wakati wa uchaguzi uliopita wa mwaka 2019, waangalizi wa kikanda walisema kulikuwa na dosari nyingi na matokeo ya kura hiyo yalipungukiwa uhalali. **VOA, DW**

# WASHINDI TWENDE ZETU IVORY COAST KI-VIP WAONDOKA NCHINI

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI wawili, Nasibu Stanford wa Dar es Salaam na Elias Athuman Simba wa kampeni ya 'Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP', wameondoka nchini kwenda Ivory Coast kushuhudia Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon), zinazoendelea.

**Mkuu wa msafara huo, Juvenalius Rugambwa, ambaye pia ni Afisa Habari wa Betika, ameliaambia Nipashe jana kuwa huo ni msafara wa kwanza ambao kampuni hiyo inawapeleka kushuhudia fainali hizo.**

Alisema washindi hao ni wa droo kubwa ya Twende Zetu Ivory Coast, ambayo inawapeleka watu sita kushuhudia fainali hizo.

"Washindi hao wataishuhudia mubashara Timu ya Tanzania (Taifa Stars), ambayo kesho Januari 17, itacheza dhidi ya Morocco.

"Kundi la kwanza litaangalia mechi hiyo laivu na kundi la pili litashuhudia ile ya Stars dhidi ya Zambia," alisema Rugambwa.

Alisema msafara wa kwanza tayari umewasili Ivory Coast na ule wa pili wa watu wanne utakwenda kabla ya mechi ya Stars na Zambia.

Rugambwa alisema tayari mwakilishi wa Betika yupo nchini humo kuwaandalia mapokezi mazuri na washindi hao watapokelewa Ki-VIP wakiwa huko na kushuhudia mechi hiyo kwa hadhi ya kivip.

"Hawa ni washindi wa droo kubwa ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP, walichofanya ni kuweka pesa kwenye akaunti zao za Tigopesa na kubeti na Betika," alisema.




Washindi wa Kampeni ya 'Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP', Elias Athumani (kushoto) na Nasibu Stanford (katikati) wakiwa tayari kuanza safari kwenda kuishangilia Taifa Stars katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON). Kulia ni Mkuu wa msafara kutoka Betika Tanzania, Rugambwa Juvelinaus. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Kwa nyakati tofauti, washindi hao walisema wanakwenda Ivory Coast kwa kazi moja tu, kuisapoti kwa kuishangilia Stars. Mbali na droo kubwa, kampeni hiyo pia ilihusisha droo ndogo iliyotoa runinga ya nchi 70, dishi na dekoda yenye kifurushi kila wiki kwa washindi wawili na pesa taslimu kila siku.

Wiki ya kwanza ilitoa washindi wawili kutoka Dodoma, wiki ya pili washindi kutoka Tanga na Lindi pia walikabidhiwa zawadi zao na wiki ya tatu washindi kutoka Pwani walikabidhiwa zawadi hizo huku wiki ya nne washindi wa Morogoro na Dar es Salaam walikabidhiwa zawadi zao kwenye droo ndogo.

Stars inashiriki Afcon kwa mara ya tatu katika historia ya michuano hiyo, baada ya ile ya 1980 nchini Nigeria na 2019 nchini Misri.

# Tigo yaahidi makubwa Kili Marathon 2024

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo ambao ni wadhamini wa mbio za Km 21-Tigo (Kili Half Marathon) za Kilimanjaro Premium Lager International Marathon, imeahidi washiriki na mashabiki uzoefu wa ina yake na wa kusisimua wakati wa tukio hilo mwezi ujao.

Ahadi hiyo inakuja takriban mwezi mmoja kabla la mbio hizo kubwa zinazotarajiwa kufanyika Jumapili ya Februari 25, mwaka huu katika Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi. Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, alisema mipango yote imekamilika na kwamba wanatarajia washiriki wengi zaidi na mashabiki katika mbio za Tigo Kili Half Marathon.

"Watanzania wengi sasa hivi wanazingatia mazoezi kama sehemu ya maisha na tumeona wengi wakishiriki katika marathon tofauti ikiwamo Kilimanjaro International Marathon ambazo zimejizolea umaarufu mkubwa ndani na nje ya nchi," alisema.

Alisema washiriki na mashabiki wategemee mtandao bora zaidi na wenye spidi ya hali ya juu wakati wa mbio hizo.

"Washiriki na mashabiki hupenda kupiga picha na kuchukua video ili kuwatumia ndugu na marafiki na kurusha mitandaoni. Tunawahakikishia uzoefu wa aina yake katika mtandao wetu ulioboreshwa," alisema.

Aliendelea kusema kuwa Tigo imekuwa mstari wa mbele katika kukuza na kutangaza utalii kupitia michezo yaani 'sports tourism' na riadha kwa ujumla na jambo hili limewafanya wawe wadhamini wa Tigo Kili Half International Marathon kwa mwaka wa tisa mfululizo.

Alisema usajili bado unaendelea kwa njia ya Tigopesa kwa mbio zote yaani km 42, 21 na tano. Washiriki wanaweza kupiga.

"Nafasi ni chache mno kwa hivyo natoa rai kwa washiriki wakamilishe usajili mara moja ili kuepuka kukosa namba kwani nafasi zikijaa waandaaji watalazimika kufunga usajili," alisema.

Wadhamini wa tukio la mwaka huu ni Kilimanjaro Premium Lager- Km 42, Tigo- Km 21 (Half Marathon), Gee Soseji - Km 5 (Fun Run). Wadhamini wa meza za maji ni Simba Cement, Kilimanjaro Water, TPC Sugar, TotalEnergies na CRDB Bank. Wabia rasmi ni -KiliMedair, Garda World Security, CMC Automobiles, Sal Salinero Hotel na wasambazaji wakuu ni - Kibo Palace Hotel na Keys Hotel.

# Mlandege sasa wageukia Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA wa Michuano ya Kombe la Mapinduzi, Mlandege FC, wamesema sasa wamegeukia maandalizi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar inayotarajiwa kurejea hivi karibuni.

Mlandege FC ambayo Jumamosi iliyopita ilibeba Kombe la Mapinduzi kwa kuifunga Simba bao 1-0 kwenye mchezo wa fainali uliopigwa Uwanja wa New Amaan Sports Complex, visiwani hapa, ipo nafasi ya saba katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 19 baada ya kushinda michezo minne, kupoteza minne na sare saba kati ya michezo 15 iliyocheza mzunguko wa kwanza.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Jaala Abdalla, alisema kupitia michuano hiyo ya Kombe la Mapinduzi wachezaji wake wamepata mazoezi na uzoefu ambao utawasaidia kukabiliana katika michezo ya Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema matumaini yake ni kuona timu hiyo inafanya vizuri kwenye Ligi Kuu Zanzibar tofauti na mzunguko wa kwanza, kwani wamefanya usajili mzuri katika kipindi hiki cha dirisha dogo.

Alisema viongozi wa timu hiyo walifanya usajili kulingana na mahitaji ya mwalimu wa timu hiyo ambaye alihitaji wachezaji ambao wataweza kuisaidia timu kutwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi pamoja na kufanya vizuri mzunguko wa lala salama wa Ligi Kuu Zanzibar.

"Lengo letu la kwanza kwa msimu huu tumefainikiwa, ambalo lilikuwa kutetea taji letu la Mapinduzi, bado lengo moja la kuhakikisha tunafanikiwa kumaliza Ligi Kuu Zanzibar tukiwa katika timu nne za juu katika msimamo wa Ligi," alisema.

Aidha, alisema timu hiyo katika kuendelea kukiimarisha kikosi chake, wanatarajia kucheza michezo mingi ya kirafiki dhidi ya timu za madaraja tofauti ili kuhakikisha wanaanza mzunguko wa pili kwa kupata matokeo mazuri.

Alisema michezo hiyo ya kirafiki itaendelea kuwasaidia wachezaji wake kujiandaa vema na kutumia mbinu mpya ambazo wamezipata kutoka kwa timu walizocheza nazo katika michuano ya Kombe la Mapinduzi.

## ZISIKUPITE

### GUIRASSY AWINDWA UNITED

KLABU za Manchester United, Newcastle na AC Milan, zinawania kumsajili mshambuliaji wa Stuttgart na Guinea, Serhou Guirassy mwenye umri wa miaka 27. ***(Football Insider)***

### YORO ATAKIWA LIVER

LIVERPOOL, Real Madrid na Paris St-Germain zinavutiwa na beki wa Lille ya Ufaransa aliye chini ya umri wa miaka 21, Leny Yoro mwenye umri wa miaka 18. ***(Telefoot)***

### BARCO ATUA BRIGHTON

KLABU ya Brighton imekamilisha usajili wa beki wa pembeni wa Argentina, Valentin Barco mwenye umri wa miaka 19 kutoka Boca Juniors kwa pauni milioni 8. ***(Telegraph)***

### MARTIAL AIKATAA SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Anthony Martial yuko tayari kukataa ofa ya Saudi Arabia kwani angependelea kusalia Ulaya, huku West Ham, Inter Milan na Fenerbahce wakihusishwa na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 28. ***(Caught Offside)***

### ARSENAL, CHELSEA AFCON

ARSENAL na Chelsea watamtazama beki wa Sporting Lisbon mwenye umri wa miaka 20, kutoka Ivory Coast, Ousmane Diomande, katika Kombe la Mataifa ya Afrika (afcon) kwa nia ya kutaka huduma zake ***(Record)***

### BENZEMA HAKIELEWEKI

MUSTAKABALI wa Karim Benzema katika Klabu ya Al-Ittihad haujulikani baada ya mshambuliaji huyo wa zamani wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 36, kukosa mazoezi na hatimaye kutengwa kwenye kambi ya klabu hiyo ya majira ya baridi kali huko Dubai. ***(Marca)***

### GIMENEZ ANYATIWA SPURS

KLABU za Tottenham, Arsenal na Fulham ziko tayari kumenyana na West Ham katika uhamisho wa majira ya joto kwa mshambuliaji wa Feyenoord mwenye umri wa miaka 22, Santiago Gimenez, raia wa Mexico. ***(Football Insider)***

### CLARKE ATAJWA PALACE

WEST Ham na Crystal Palace wana nia ya kumsajili winga, Jack Clarke mwenye umri wa miaka 23, kutoka Sunderland, ambaye anakadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 20, huku klabu yake ya zamani ya Tottenham Hotspur ikitarajiwa kupata asilimia 25 ya ada yoyote ya uhamisho wake. ***(Football London)***

### FOFONA AGOMBEWA

KLABU ya Burnley inatafuta mpango wa kumnunua mshambuliaji wa Chelsea na Ivory Coast, David Datro Fofana mwenye umri wa miaka 21, ambaye ameitwa kutoka kwa mkopo Union Berlin. ***(Athletic)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# XAVI AWAOMBA RADHI MASHABIKI BARCELONA

**RIYADH,** Saudi Arabia

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez, ameomba msamaha kwa mashabiki wa klabu hiyo baada ya kuchapwa mabao 4-1 na Real Madrid Jumapili kwenye fainali ya Kombe la Supercopa nchini Saudi Arabia.

**Vinicius Junior alifunga hat-trick kipindi cha kwanza katika Uwanja wa Al-Awwal Park, mabao mawili ndani ya dakika 10 za kwanza, naye Rodrygo Goes akakamilisha kipigo hicho kipindi cha pili huku Madrid wakilipiza kisasi kwa Barca kwa kushindwa mwaka jana kwenye fainali hiyo.**

Robert Lewandowski alikuwa ameisaidia Barca kwa muda kurejea mchezoni wakati wakiwa nyuma kwa mabao 2-1, lakini bao la tatu la Vinicius, kupitia mkwaju wa penalti, liliondoa matumaini kabla ya mapumziko.

"Nimesikitishwa na nina huzuni," alisema akiiambia Movistar baada ya mechi.

"Hili ni soka na leo tunapaswa kukabiliana na upande mchungu wa mchezo.

"Ni aibu, tulikuwa na matumaini makubwa kwenda fainali na tumetoa matokeo mabaya zaidi. Tulianza vibaya, tulipata nafasi ya kurejea, lakini penalti iliua mchezo.

"Hatukuwa na raha. Madrid walifanya uharibifu mkubwa kwenye kaunta na katika kipindi cha mpito. Tunaomba radhi kwa mashabiki, hatukushindana, lakini nimepata vipigo vingi na klabu hii."

Xavi aliomba msamaha kutoka kwa mashabiki mara kadhaa katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo na akasema yuko tayari kwa ukosoaji ambao "utastahili" kufuata.

"Ni wakati wa kusema pole kwa mashabiki na kukubali ukosoaji unaokuja," aliongeza. "Hatukuonesha upande wa timu ambayo tunapaswa kuwa nayo kwenye fainali, haswa dhidi ya Madrid.

"Tulikuwa katika hali mbaya zaidi na ni kombe lililopotea. Ninawajibika. Ninakubali kukosolewa na tutaendelea kufanya kazi kwa bidii.

## ●●● Ni kushindwa kugumu, Madrid walifanya uharibifu mkubwa kwenye...

"Ni kushindwa kugumu, lakini tumepona kutoka kwa kushindwa mara nyingi hapo awali na tutashindana tena kwa njia bora zaidi."

Hata hivyo, licha ya hali ya matokeo hayo, pamoja na kuwa nyuma kwa pointi nane kwa vinara wa La-Liga, Girona, Xavi, ambaye aliiongoza Barca kutwaa ubingwa wa ligi mwaka jana, hahofii kibarua chake.

"(Kuna kujiamini, ndio," alisema bosi wa Barca, ambaye aliongeza mkataba wake hadi 2025 mwaka jana, alisema alipoulizwa kama bado anaungwa mkono na uongozi wa klabu.

"Lazima tujikosoe na kusahihisha mengi, lakini bado naamini katika mradi huo na unaweza kuwa na msimu mzuri. Tunapaswa kujikosoa sana juu ya utendaji wetu leo.

"Kuna sababu za kuamini, tulishinda mataji mawili mwaka jana nikiwa kocha, si zamani, ilikuwa ngumu naomba radhi kwa mashabiki, lakini kuna mabishano ya upande wetu."

# VINICIUS JR: MIMI SI MTAKATIFU




**RIYADH,** Saudi Arabia

NYOTA Vinicius Junior ametetea tabia yake ya uwanjani baada ya kufunga hat-trick katika ushindi wa mabao 4-1 wa Real Madrid dhidi ya Barcelona kwenye fainali ya Supercopa ya Hispania, huku akikiri "mimi si mtakatifu."

Mshambulizi huyo wa Brazil alifunga mabao mawili katika dakika kumi za kwanza na kuiweka Madrid kileleni mjini Riyadh, kabla ya Robert Lewandowski kuwajibia Barca.

Vinicius aliongeza bao la tatu kwa mkwaju wa penalti kabla ya muda wa mapumziko na Rodrygo Goes akafunga la nne kabla ya Ronald Araujo kutolewa nje kwa kadi nyekundu.

Hata hivyo, Vinicius pia aligombana na benchi la Barca, huku kamera za runinga zikimwonesha akifanya ishara ya '4-1' kuelekea kwao, akionesha matokeo, mwishoni mwa mchezo.

"Inanihuzunisha. Kila mtu anataka kupigana nami, kwa sababu wanajua itakuwa 'Vini alifanya hivi, Vini alifanya vile' kwenye vyombo vya habari," alisema Vinicius katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi na kutajwa mchezaji bora wa fainali hiyo.

"Ninajaribu kuwa mtulivu na kuzingatia kufanya vizuri iwezekanavyo. Si juu yangu tu.

"Bila shaka, mimi si mtakatifu," aliongeza. "Wakati mwingine mimi huongea sana, wakati mwingine napiga chenga wakati sistahili. Lakini niko hapa ili kuboresha, na kuwa mfano wa kuigwa kwa watoto. Nataka kuimarika."

Vinicius alisherehekea bao lake la kwanza kwa kuiga alama ya Cristiano Ronaldo, huku Supercopa ikichezwa kwenye Uwanja wa Al-Awwal Park, nyumbani kwa Al-Nassr ya Ronaldo.

"Sherehe ilikuwa ya Cris," alisema Vinicius.

"Yeye ni sanamu yangu, na anacheza hapa sasa... nimefurahishwa sana na tulichokifanya leo (juzi). Kuifunga Barcelona si rahisi na kushinda 4-1 ni vigumu.

## Kane atabiriwa kuvunja rekodi ya Lewandowski

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel, amesema Harry Kane ana uwezo wa kuvunja rekodi ya Robert Lewandowski ya msimu mmoja wa Bundesliga kufunga mabao 41 huku mshambuliaji huyo wa England akiendelea kufurahia msimu mzuri wa kwanza nchini Ujerumani.

Lewandowski aliweka historia Mei 2021 alipovunja rekodi ya msimu mmoja ya Gerd Müller, ambayo ilidumu kwa miaka 39.

Kane alifunga bao lake la 22 la Bundesliga msimu huu katika dakika za mwisho za ushindi wa 3-0 wa Bayern dhidi ya Hoffenheim Ijumaa - ingawa lazima afunge mabao 19 katika mechi 16 zilizosalia za Bayern ili kufikia rekodi hiyo.

"Iko hatarini," Tuchel aliiambia ESPN alipoulizwa kama Kane anaweza kuvunja rekodi ya Lewandowski.

"Hakuna mtu ambaye angeweza kuamini kwamba itakuwa hatarini, lakini iko hatarini. Tunahitaji bahati kidogo. Tunahitaji timu kuendelea, Harry anahitaji kuwa fiti, na kisha tuone kile kinachokuja... kwa uwazi. fikiria kwamba kwa Harry hakuna kikomo."





## Ajax yathibitisha kumtaka Henderson

**AMSTERDAM,** Uholanzi

KOCHA wa Ajax, John van 't Schip, amethibitisha nia ya klabu hiyo kutaka kumsajili nahodha wa zamani wa Liverpool, Jordan Henderson.

Vyanzo viliiambia ESPN mapema wiki hii kwamba Henderson, ambaye hana furaha kule Saudi Arabia, anasakwa na Ajax pamoja na timu za Ligi Kuu England na Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Akizungumza kabla ya mechi ya Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, dhidi ya Go Ahead Eagles, Van 't Schip aliiambia ESPN kwamba mazungumzo yanaendelea kuhusu uhamisho huo.

"Kuna mazungumzo mazito yanaendelea na Henderson," alisema Van 't Schip. "Bado ana baadhi ya mambo ya kupanga huko Saudi Arabia.

"Si siri kwamba tunaweza kumtumia mchezaji wa aina hiyo. Vijana wengine wanaweza kufaidika kwa hilo."

Lakini chanzo kiliiambia ESPN kwamba Al Ettifaq inaweza kutokuwa na nia ya kumruhusu kiungo huyo mkongwe kuondoka miezi michache tu baada ya kumsajili.

Henderson mwenye umri wa miaka 33, alihamia Saudi Pro League kutoka Liverpool Julai 2023, na kumaliza kukaa kwa miaka 12 pale Anfield na kumfanya kushinda Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la FA, UEFA Super Cup na Kombe la Klabu Bingwa Dunia.

Hata hivyo, Al Ettifaq wanasita kumwona mchezaji huyo wa Kimataifa wa England akiondoka kwani inaweza kuathiri sifa si tu ya klabu bali hata ligi.

Ajax wako tayari kulipa ada ndogo ya uhamisho, lakini hawana nia ya uhamisho wa mkopo, chanzo kiliiambia ESPN.

# IHEFU KAMILI ARUSHA, YAZOA MASTAA KUTOKA SINGIDA FG

Na Oliver Albert

IHEFU tayari ipo jijini Arusha ilikohamishia makazi yake kutoka Mbarali Mbeya huku Kocha wa kikosi hicho, Mecky Maxime, akisema watarudi na moto Ligi Kuu Bara ikirejea kwa kuwa wanataka kumaliza nafasi za juu.

**Inadaiwa Ihefu imenunuliwa na kigogo mmoja wa serikali na maskani yake kwa sasa yatakuwa jijini Arusha.**

Katika dirisha dogo ambalo lilitarajiwa kufungwa jana usiku, tayari Ihefu ilishakamisha usajili wa Manu Labota kutoka FC Lupopo ya Congo, Joash Onyango, Bruno Gomes, Elvis Rupia, Marouf Tchakei, Kevin Nashon na Aboubakary Khomein wote kutoka Singida Fountain Gate.

Pia inaelezwa wakati wowote timu hiyo itamstambulisha kocha wa zamani wa Mbeya City na Singida United, Mathias Lule, ili kusaidiana na Kocha Mkuu, Maxime.

Maxime amesema tayari wameshaanza mazoezi kwenye makao yao mapya jijini Arusha na wachezaji wote wana ari kubwa.

"Tunashukuru tumefika salama Arusha na kupokelewa vizuri na wakazi wa hapa na naamini watatupa ushirikiano ligi ikirejea na tunawaahidi hatutawaangusha.

"Asilimia kubwa ya wachezaji wapo hapa na baadhi tu bado hawajawasili kutokana na dharura, lakini naamini hadi mwisho wa wiki kikosi kitakuwa kimekamilika," alisema Maxime.

Alisema anamini wachezaji walioongezwa kikosini wataongeza chachu ya kupata matokeo mazuri katika mechi zijazo.

"Hatuko katika nafasi nzuri, lakini naamini ligi ikirejea tutakuja kivingine na tutahakikisha tunapambana kadri ya uwezo wetu ili kuleta ushindani na ili kusogea nafasi za juu.

"Uwezo tunao na tuna wachezaji wazuri ambao kama wakijitoa na kuipambania timu, tunaweza kutoka nafasi tuliyopo na kupanda juu na ikiwezekana hata kupata nafasi ya kucheza kimataifa.



Vijana wanaolelewa katika Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete (JK Park), wakiwania mpira wakati wa mazoezi katika viwanja vya kituo hicho jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Taifa Wasichana U-17 waitwa kuiwinda Zambia

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wasichana chini miaka 17 (U-17), Bakari Shime, ametangaza kikosi cha wachezaji 25 kitakachoingia kambini Januari 20, mwaka huu, kujiandaa na mchezo wa kuwania kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Zambia.

Kikosi kilichotangazwa ni makipa; Marian Shaban, Mwanaidi Maulid (Bunda Queens) na Salome Saint (Geita Gold Queens). Mabeki ni Sarah Joel, Manka Richard (Fountain Gate Princess), Neema Damas (Baobab Queens), Edna Makamba (Oysterbay Queens), Ladia Maximilian (JKT Queens), Masika Mwakisua (Yanga Princess), Sarah Lucas na Kurwa Rockets (Bunda Queens).

Viungo ni Winifred John (Yanga Princess), Ester Maseke, Melikia William, Semeni Juma (Bunda Queens), Naomi Charles, Sabina Alex, Asha Ramadhani (Geita Gold Queens) na Marry Siyame (Laliga Academy- Hispania). Washambuliaji ni Jamil Rajabu, Yasinta Mitoga, Winifrida Gerald, Mwantima Mwarabu (Geita Gold Queens) na Jamil Celestine (Bunda Queens).

Kocha Shime ameliambia Nipashe kuwa kikosi hicho cha wachezaji 25, kitaingia kambini rasmi Januari 21 kujiandaa na mchezo dhidi ya Zambia ambao utapigwa Februari 2, mwaka huu nchini humo.

Alisema wanatambua umuhimu wa mchezo huo na wanaingia kambini mapema kujiandaa na mchezo dhidi ya Zambia, ambao utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu ya ubora wa vikosi cha timu zote.

"Kuhusu mechi za kirafiki kwa sasa siwezi kusema nitacheza ngapi kwa sababu bado sijaomba kwa uongozi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), kutafutiwa timu lakini kama itatokea kuna timu itahitaji nitakuwa tayari," alisema Shime.

**Kocha Shime ameliambia Nipashe kuwa kikosi hicho cha wachezaji 25, kitaingia kambini rasmi Januari 21...**

# Rekodi za straika

INATOKA UKURASA 24

la Mapinduzi kwani imempa nafasi ya kujua mchezaji gani wa kubaki na wa kuondoka yeye mwenyewe bila kuambiwa na mtu.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally amesema licha ya kutopata ubingwa, lakini kocha wao Benchikha ameonekana kuyafurahia mashindano hayo kwani ameshuhudia mwenyewe kwa macho yake viwango vya wachezaji wake wote, hivyo atafanya maamuzi yeye mwenyewe.

"Benchika amesema amepata muda mrefu wa kuwaona wachezaji wake na hasa wale ambao wamekuwa hawapati namba kwenye kikosi cha kwanza, ametuambia amemwona Luis Miqussone akirejea kwenye kiwango na pia amepata muda wa kumtazama Hussein Kazi akisema ni hazina, lakini amesema kuna wachezaji ambao hajaridhika nao na atawaacha.

"Hii yote ni kwa sababu ya michuano ya Kombe la Mapinduzi, vinginevyo sijui ingekuwaje, kwa hiyo kaeni mkao wa kujua tukaoachana nao, tayari mwalimu amewapa nafasi baadhi ya wachezaji na amejiridhisha kuwa hawawezi kumsaidia kwenye safari yake huko mbele," alisema Ahmed.

# Moloko apisha straika

INATOKA UKURASA 24

kusajili mshambuliaji, tayari tumeshakamilisha usajili wake na atakuwa sehemu ya kikosi cha timu yetu kipindi chote cha mkataba wake," alisema Kamwe.

Alieleza kuwa tayari kuna baadhi ya wachezaji wametolewa kwa mkopo kulingana na mapendekezo ya kocha Gamondi na kupisha usajili mpya.

Katika hatua nyingine umeweka wazi kuachana na winga Mkongomani, Moloko kwa makubali ya pande zote mbili,

Yanga imefikia hatua hiyo baada ya nyota huyo kukosa nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Kocha Miguel Gamondi.

Moloko alikuwa kwenye kikosi cha Yanga kilichoshiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi 2024 na kutolewa hatua ya robo fainali kwa kipigo cha mabao 1-3 dhidi ya APR FC.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, wamechukua maamuzi ya kuachana na winga huyo kutokana na makubaliano ya pande zote mbili ili kupisha nafasi ya usajili mpya kuingia.

# Michezo

Jumanne Januari 16, 2024

Nipashe




Twende Zetu Ivory Coast KI-VIP waondoka UKURASA 20

# REKODI STRAIKA MGAMBIA SIMBA HIZI HAPA

Na Adam Fungamwango

## Mwenyewe aahidi mabao, sasa mtihani kwa Benchikha, ambaye anata...

KATIKA dakika za mwisho za uhamisho wa dirisha dogo la usajili, Klabu ya Simba imetangaza kumsajili straika Pa Omar Jobe (25), raia wa Gambia kwa mkataba wa miaka miwili akitokea katika Klabu ya FC Zhenis ya Kazakhstan, rekodi zake zikionesha kuwa amefunga mabao 41 katika mechi 73, akichezea klabu tano tofauti.

**Straika huyo amesajiliwa siku moja tu baada ya Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha kulalamika kuwa kwa sasa anakosa mshambuliaji mwenye uwezo wa kupachika mabao na mwenye nguvu ya kukabiliana na mabeki wababe ndani ya eneo la hatari.**



Pa Omar Jobe

Rekodi zinaonesha kuwa Jobe alifunga mabao 23 na 'asisti' tano, katika mechi 28 kwenye Ligi Kuu ya Bangladesh. Katika Ligi Kuu ya Kazakhstan akifunga mabao 13 na 'asisti' tano katika michezo 25 aliyocheza.

Jobe akiwa katika Ligi Kuu ya Macedonia Kaskazini alifunga mabao matatu katika mechi 12 wakati kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kabla ya kutua timu hiyo ya Ulaya alifunga mabao mawili katika mechi nne huku Ligi ya Mabingwa Afrika akiwa hajaziona nyavu katika michezo miwilii aliyocheza.

Katika maisha yake ya soka, klabu alizozichezea Jobe ni pamoja na Shkendija na Struga za nchini Macedonia, msimu wa 2022/23 alijiunga na Klabu ya Neman Grodno ya nchini Beralus kabla ya kujiunga na Zhenis na sasa Simba.

Kabla ya hapo, Mgambia huyo alianza kuzichezea Klabu za Tallinding United FC ya nchini mwao, 2011 hadi 2014, alipotimkia kwenye Klabu ya ASEC Ndiambour ya Senegal, 2017 hadi 2019 ambapo alicheza michuano ya Afrika Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho.

Akizungumza wakati akitambulishwa Simba, Jobe hakuwa na maneno mengi zaidi ya kusema "nipo hapa kwa ajili ya kufunga mabao".

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu hiyo, Salim Abdallah 'Try Again', amesema wameongeza mchezaji mwingine wa nafasi hiyo kwa ajili ya kuongeza nguvu na kuwasukuma waliopo ili waweze kufanya vizuri.

"Tumeongeza mchezaji mwingine wa nafasi ya ushambuliaji kuja kuongeza nguvu katika eneo hilo tunamkaribisha sana Jobe," alisema Try Again.

Kusajiliwa kwa straika huyo kutafanya safu ya ushambuliaji ya Simba kuwa na mastraika wanne, na kumpa wigo mpaka kocha, ambapo kwa sasa ina nahodha John Bocco, Jean Baleke na Moses Phiri.

Hata hivyo, kwa siku za karibuni, mastraika hao wote wameonekana kutokuwa kwenye kiwango chao cha kawaida kiasi cha kumfanya Benchikha kulalamika kupatiwa straika mwingine haraka.

Wakati huo huo, Klabu ya Simba imesema kocha wao Benchikha ameonekana kufurahishwa na michuano ya Kombe

INAENDELEA UKURASA 23

# Moloko apisha straika Yanga

Na Saada Akida

WAKATI uongozi wa Klabu ya Yanga ukisema umesikia kilio cha mashabiki wao kuhusu kuimarisha safu yao ya ushambuliaji na umeshusha mshambuliaji mwenye uwezo wa hali ya juu katika kipindi hiki cha dirisha dogo lililofungwa jana usiku, pia umetangaza kuachana na winga wao, Jesus Moloko kwa makubaliano ya pande zote mbili.

Straika huyo ambaye amesajiliwa muda mfupi kabla ya dirisha la usajili kufungwa jana usiku, alitarajiwa kutambulishwa wakati wowote kuanzia jana usiku wa manane kama ilivyokuwa kwa kiungo mshambuliaji, Stephane Aziz Ki mwaka 2022.

Tayari Yanga ilifanya usajili wa dirisha dogo kwa kutambulisha nyota wawili; Shekhan Ibrahim kutoka JKU FC ya visiwani Zanzibar na Augustine Okrah aliyewahi kuitumikia Simba msimu uliopita.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wamefanya mabadiliko machache kwa kufuata mapendekezo ya Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, kwa kuimarisha safu ya ushambuliaji.

Alisema wamesikia kilio cha benchi la ufundi na mashabiki wa timu hiyo kuhakikisha katika usajili huu wanaimarisha safu ya ushambuliaji kwa kuleta mtu hatari.

"Ni kweli tumefanya kazi tuliyotumwa na kusikililiza kilio cha kocha Gamondi pamoja na mashabiki wetu juu ya

INAENDELEA UKURASA 23



Jesus Moloko



9 770856 541002 >